**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MKOA WA ARUSHA

# KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (Regional Consultative Committee – RCC) WA ARUSHA CHA TAREHE 16/02/2017 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA WA ARUSHA


***Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,***
***S.L.P. 3050,***
***ARUSHA.***
***Simu Na. 250 2270/2502272/2502289.***
***Fax 2545239/2544386***
***E–mail: rasarusha@pmoralg.go.tz, ras.arusha@tamisemi.go.tz***


***FEBRUARI, 2017***

# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (REGIONAL CONSULTATIVE COMMITTEE – RCC) WA ARUSHA KILICHOFANYIKA TAREHE 21/10/2016 KATIKA UKUMBI WA MKUU WA MKOA WA ARUSHA

## MUHT. NA. 1 – WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mrisho Mashaka Gambo | - Mkuu wa Mkoa | -Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Richard N. Kwitega | - KatibuTawala Mkoa | -Katibu |
| 3. | Mhe. Daniel T. Ole Nasha | - Mbunge Ngorongoro | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Julius K. Laiser | - Mbunge Monduli | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. Godbless Lema | - Mbunge Arusha | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. Willy Qambalo | - Mbunge Karatu | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. Cecilia D. Pareso | - Mbunge Viti Maalum | -Mjumbe |
| 8. | Mhe.Catherine Magige | - Mbunge viti Maalum | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. Joyce Mukya | - Mbunge Viti maalum | -Mjumbe |
| 10. | Mhe. Iddi H. kimanta | - Mkuu wa Wilaya Monduli | -Mjumbe |
| 11. | Mhe. Gabriel F. Daqarro | - Mkuu wa Wilaya Arusha | -Mjumbe |
| 12. | Mhe. Alexander P. Mnyeti | - Mkuu wa Wilaya Arumeru | -Mjumbe |
| 13. | Mhe. Daniel G. Chongolo | - Mkuu wa Wilaya Longido | -Mjumbe |
| 14. | Mhe. Theresia J. Mahongo | - Mkuu wa Wilaya Karatu | -Mjumbe |
| 15. | Mhe. Rashid M. Taka | - Mkuu wa Wilaya Ngorongoro | -Mjumbe |
| 16. | Mhe. Kalisti Lazaro | - Meya Jiji la Arusha | -Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mathew E. Siloma | - Mwenyekiti H/W ya Ngorongoro | -Mjumbe |
| 18. | Mhe. Kenedy S. Olemoleit | - Mwenyekiti H/W ya Longido | -Mjumbe |
| 19. | Mhe. Willy J. Njau | - Mwenyekiti H/W ya Meru | -Mjumbe |
| 20. | Mhe. Noah Lembris Saputu | - Mwenyekiti H/W ya Arusha | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Jublate G. Mnyenye | - Mwenyekiti H/W ya Karatu | -Mjumbe |
| 22. | Mhe. Isack J. Copriano | - Mwenyekiti H/W ya Monduli | -Mjumbe |
| 23. | Mhe. Waziri Mourice | - Mkurugenzi H/W ya karatu | -Mjumbe |
| 24. | Bw. Raphael J. Siumbu | - Mkurugenzi H/W ya Ngorongoro | -Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 25. | Dkt.Wilson M. Charles | - Mkurugenzi H/W ya Arusha | -Mjumbe |
| 26. | Bw. Jumaa Mhina | - Mkurugenzi H/W ya Longido | -Mjumbe |
| 27. | Bw. Stephen A. Ulaya | - Mkurugenzi H/W ya Monduli | -Mjumbe |
| 28. | Bw. Athumani J. Kihamia | - Mkurugenzi Jiji la Arusha | -Mjumbe |
| 29. | Bw. Christopher J. Kazeri | - Mkurugenzi H/W ya Meru | -Mjumbe |

**MUHT. NA. 2 – WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA:**

1. Mhe. Joshua Nassari – Mbunge Jimbo la Arumeru Mashariki
2. Mhe. Gibson Ole Meisieki – Mbunge Jimbo la Arumeru Magharibi
3. Mhe. Amina Mollel – Mbunge Viti Maalum

**MUHT. NA. 3 – KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

1. Bw. Patrick Mwakalobo - Afisa Usalama Mkoa
2. Bw. Salvin Frank Elius - D.C. Police
3. Bw. Shukuru A. Ndupe - Afisa Usalama wa Arusha
4. Bw. Basil Likasi - Kaimu Afisa Uhamiaji Mkoa
5. Bw. Hezron H. Nganoga - Kny: Afisa Magereza Mkoa
6. Bi. Jacqueline Kapila - PCCB Mkoa

## MUHT. NA. 4 – WAALIKWA WALIOHUDHURIA:

### (i) MAAFISA KUTOKA TAASISI MBALIMBALI

1. Bw. Johany Kachwamba - Afisa Habari - TANESCO TGDC
2. Shakiru Idrissa Kajitugus - Meneja Mipango na Miradi - TANESCO
3. Bibi Anicia Ng'weshemi - Meneja Mkoa - NHIF
4. Aliko Mwanusako - NBC Arusha Branch
5. Eng. Ruth S. Koya - AUWSA
6. Bw. Patrick E. Shoo - HESLB
7. Bw. Sunday Charles - HESLB
8. Bibi Ruth Mnzava - Utafiti Seliani
9. Bw. Valery Sonola - LITA Tengeru
10. Bibi Anna A. Mbasha - Maadili ya Viongozi wa Umma - ARUSHA
11. Dr. Maduhu Kazi - BOT
12. Bw. Peter Bayp - ANGONET
13. Bw. Ernest Ndunguru - BOT
14. Bw. Gasper Mlingwa - TANESCO
15. Eng. J. Dekalupale - TANROADS

16. Bw. Elibariki Malley - ANGONET
17. Bw. Allan J.H. Kijazi - TANAPA
18. Bw. Kalutu P.R Koshuma - TEMDO
19. Bw. Israel H. Naman - Ngorongoro Conservation

**(ii) MAKATIBU TAWALA WASAIDIZI NA WAKUU WA VITENGO, SECRETARIET YA MKOA WA ARUSHA**

1. Bw. Anza Amen Ndossa - Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Mipango na Uratibu
2. Bw. Hamadany Z. Mansur - Katibu Tawala msaidizi Huduma za Miundo Mbinu
3. Bibi Suzan Mnafe - Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Serikali za Mitaa
4. Eng. Joseph E. Makaidi - Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Maji
5. Dr. Frida Mokiti - Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Afya
6. Bw. H. Chitukuro - Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Uchumi na Uzalishaji
7. David Lyamongi - Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Rasilimaliwatu na Utawala
8. Bw. Albert M. Nestory - Katibu Tawala Msaidizi - Elimu
9. Bw. Elirehema Z. Masanja - Mkuu wa Kitengo cha Ugavi
10. Bw. Furaha B. Songa - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
11. Bw. Philbert Mlihano - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani

**(iii) MAKATIBU TAWALA WILAYA**

1. Bw. Abbas Kayanda - Katibu Tawala, Wilaya ya Karatu
2. Bw. Toba A. Nguviga - Katibu Tawala, Wilaya ya Longido
3. Bw. Robert Siyantemi Amos - Katibu Tawala, Wilaya ya Monduli
4. Bw. Lemueli Christian Kuto - Katibu Tawala, Wilaya ya Ngorongoro
5. Bw. Nyangusi L. Nailiba - Kaimu Katibu Tawala, Wilaya ya Arumeru

**(iv) MAAFISA KUTOKA HALMASHAURI ZA WILAYA**

1. Bw. Peter Ngussa - Mchumi Halmashauri ya Arusha
2. Bibi Joan S. Foya - Afisa Mipango H/W ya Longido
3. Bw. H. Singano - Afisa Mipango HW ya Meru

**(v) WATAALAMU WA SEKRETARIET YA MKOA**

1. Bw. Yotham Ndembeka - Katibu wa Mkuu wa Mkoa
2. Bw. Daniel Loiruki - Afisa Kilimo

3. Bibi Blandina Nkini - Afisa Maendeleo ya Jamii Mkuu
4. Bibi Susan Ngulubai - Mchumi
5. Bibi Grace Mbaruku - Mchumi Mkuu
6. Bibi Erena Materu - Afisa Maendeleo ya Jamii
7. Swalehe M. Ally - AfisaItifaki
8. Dr. Sabas P. Shange - Afisa Mifugo
9. Dr. Jacquline Urio - Mganga Mfawidhi, Hospitali ya Mkoa, Mt. Meru
10. Bw. Peter Laswai - Afisa Ushirika
11. Bw. Muhsin Kassim - Itifaki
12. Bw. Emanuel F. Bariki - TEHAMA
13. Henry R. Nyamkama - Mhasibu
14. Bibi Lilian Lyakurwa - Katibu Muhtasi
15. Bibi Melania Kapungu - Mhudumu
16. Bi. Grace J. Bundala - Mhudumu

**(V) VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA**

1. Mhe. Michael L. Laizer - Chama cha Mapinduzi
2. Mhe. Kisanyage Innocent J. - CHADEMA
3. Mhe. Abdallah Shaaban said - CUF
4. Mhe. Feruzy J. Feruzison - NRA
5. Mhe. Rajab Juma - UMD – MARS
6. Mhe. Hamad Ibrahim - ADC
7. Mhe. Mgina Ibrahim - AFP
8. Mhe. Simon Johnson - Sauti ya UMA (SAU)
9. Mhe. Simon Paul Ngilisho - Demokrasia Makini
10. Mhe. Michael N. Kivuyo - ACT
11. Mhe. Abraham M. Chipaka - NCCR MAGEUZI
12. Mhe. Makanzo - TLP
13. Mhe. Haika Willium Mkenda - CCK

(**Vii) WAANDISHI WA HABARI**

1. Bw. Khalifa Mshana - TBC
2. Bw. Amiri Ibrahim - ITV
3. Bw. Musa Juma - Mwananchi
4. Bibi Veronica Mheta - Habarileo
5. Bw. Richard Mwangulube - Jambo Leo
6. Bibi Prisca Libaga - Habarimaelezo

**(Vii) SEKRETARIET YA KIKAO**

1. Bibi Grace Mbaruku - Mchumi Mkuu
2. Bibi Blandina Nkini - Afisa Maendeleo ya Jamii Mkuu
3. Bibi Susan Ngulubayi - Mchumi
4. Bibi Erena Materu - Afisa Maendeleo ya Jamii

## AGENDA NA. 1 –MUHT. NA. 1: KUFUNGUA KIKAO:

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 7.00 mchana baada ya Katibu wa kikao kumhakikishia kuwa akidi imetimia. Kwakuwa utambulisho ulishafanyika katika kikao cha kwanza cha asubuhi kujadili migogoro ya ardhi, hivyo mwenyekiti aliwataka wajumbe kuendelea moja kwa moja na agenda za kikao bila kupoteza muda.

## AGENDA NA. 2: MUHT. NA. 2: KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO:

Wajumbe waliridhia agenda za kikao kama zilivyokuwa zimeorodheshwa bila mabadiliko yoyote kama ifuatavyo:-

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha agenda za kikao
3. Kuthibitisha kumbukumbu za kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa cha tarehe 24/03/2016
4. Taarifa ya Utekelezaji wa maazimio ya kikao cha tarehe 24/03/2016
5. Yatokanayo na Kamati za Ushauri za Wilaya
6. Maendeleo ya Sekta ya Afya
7. Maendeleo ya Sekta ya Maji
8. Maendeleo ya Sekta ya Elimu
9. Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
10. Maendeleo ya Sekta ya Mifugo
11. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2015/2016
12. Mada Maalumu
    - i. Kukabiliana na Maafa
    - ii. Usambazaji Umeme Mkoa wa Arusha
    - iii. Matumizi ya Nishati mbadala

13. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
14. Kufunga Kikao

**AGENDA NA. 3 – MUHT. NA. 3: KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA CHA TAREHE 21/10/2016**

Wajumbe wa Kamati walipitia Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 24/03/2016 na katika agenda hii kulikuwa na masahihisho kama ifuatavyo:-

Ukurasa namba mbili (2) Jina Rebeca Mgodo lisomeke Rebeca Mkodo
Ukurasa namba saba (7) neno kutolowa lisomeke kutolewa
Ukurasa namba kumi na mbili (12) kipengele namba (ix) neno makrabrsha lisomeke makabrasha.

Baada ya masahihisho hayo wajumbe waliridhia muhtasari na kukubali upitishwe.

## AGENDA NA. 4 – MUHT. NA. 4: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 21/10/2016

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimia ya kikao cha tarehe 24/03/2016 ambayo iliwasilishwa na Katibu wa kikao. Taarifa ilijadiliwa na maazimio yalitolewa kama ifuatavyo:-

**HOJA NA. 1:** Taarifa zilizotolewa nyingi hazikuwa sahihi na takwimu zake zilitiliwa mashaka na kamati

**AZIMIO NA. 1 –** Kamati ilipendekeza kuwa katika kutoa taarifa za utekelezaji wa maazimio kikao kijacho kila Halmashauri itatoa taarifa yake wenyewe kwa kufuata fomati ambayo itaelekezwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kikao. Hii ni kutokana na taarifa zinazotumwa Mkoani baadhi kuonekana hazina ukweli ndani yake wala hazina takwimu za kutosha.

## AGENDA NA. 5 – MUHT. NA. 5: YATOKANAYO NA KAMATI ZA USHAURI ZA WILAYA

Yatokanayo na Kamati za Ushauri za Wilaya yalihusiana na Migogoro ya Ardhi. Migogoro hiyo tayari ilishawasilishwa na kujadiliwa kwenye kikao cha migogoro ya Ardhi kilichofanyika tarehe 21/10/2016 kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi sa 6:00 mchana.

## AGENDA NA. 6 – MUHT.NA 6: MAENDELEO YA SEKTA YA AFYA

**HOJA NA. 2:** Taarifa ya Sekta ya Afya iliyotolewa ilieleza mazuri tu bila kuleta changamoto ambazo zinahitajika kujadiliwa na kuwekewa mikakati

**AZIMIO NA. 2:** Wajumbe walitaka taarifa ya Afya iboreshwe zaidi kwa kuongeza vipengele ambavyo vimeachwa kama Chanjo na magonjwa yasiyoambukiza lakini yamekuwa ni tishio kama vile Kansa, presha na Sukari hii itaisaidia kamati kuweka mikakati juu ya changamoto hizo.

## AGENDA NA. 7 – MUHT. NA. 7: MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI

**HOJA NA 3:** Wajumbe walisema kumekuwa na miradi mingi mno ya maji ambayo haitekelezeki, na wakandarasi wengi wameacha kazi na kuondoka eneo la mradi bila kukamilisha kazi walizopangiwa kwa mujibu wa mikataba yao.

**AZIMIO NA. 3:** Wajumbe walipendekeza kuwepo na miradi michache ya maji ambayo nguvu ya fedha itaelekezwa huko na kuweza kukamilika kwa wakati kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haitekelezeki.

## AGENDA NA. 8 – MUHT. NA. 8: MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU

**HOJA NA. 4:** Afisa Elimu Mkoa akiwasilisha mada, alieleza kuwa kuhusu tatizo la madawati Ngorongoro hakuna upungufu wa madawati, jambo ambalo wajumbe walikataa na kumwambia kuwa taarifa zake sio sahihi kwani hadi tarehe ya kikao kulikuwa na upungufu wa madawati zaidi ya 1,500. Na kuna baadhi ya shule watoto bado wanakaa chini.

**AZIMIO NA 4:** Kamati iliazimia kuwa taarifa hizo hazikuwa sahihi, na kumwagiza Afisa Elimu wa Mkoa kuleta taarifa sahihi za madawati katika kikao kijacho.

**AZIMIO NA 5:** Katibu Tawala wa Mkoa aliagizwa kufuatilia ni nani ametoa takwimu hizo ambazo si sahihi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na achukuliwe hatua za kinidhamu.

## AGENDA NA. 9 – MUHT. 9: MAENDELEO YA KILIMO:

Katika Agenda hii, kulitolewa hoja juu ya usambazaji wa Vocha kwa wakulima pamoja na pembejeo kama mbolea.

Katika hoja hii, ufafanuzi ulitolewa na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, na Uvuvi. Utaratibu wa Vocha umefutwa kwani ulikuwa ukiwajengea baadhi ya watu ulaji. Kuhusu suala la mbolea, Mhe. Naibu Waziiri alisema itasambazwa na Kampuni mpya ya mbolea ya Taifa (TFC) ambayo ina vituo 25 vya kusambaza mbolea hiyo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Na mbolea hiyo itasambazwa moja kwa moja Wilayani ambapo Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zitakuwa wasimamizi wakuu wa zoezi hilo. Aidha, pembejeo zimepungua kwa asilimia 60 ikilinganishwa na kipindi kilichopita.

Kuhusu deni la mawakala wa pembejeo kwa mwaka 2014/15 Serikali ilionekana inadaiwa shilingi Bilion 6, lakini baada ya Wizara ya Fedha kufanya uhakiki iligundua kwamba kulikuwa na wizi mkubwa kwani Serikali ilikuwa inadaiwa milioni 200 tu. Na mwaka 2015/16 Serikali ilikuwa inadaiwa Bilioni 64 na madai ya fedha hizo yamerejeshwa Wizara ya fedha kwa uhakiki zaidi ili kupata ukweli wa deni hilo.

**HOJA NA. 5:** Suala la upatikanaji wa chakula cha uhakika katika Mkoa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi, kwa sehemu kubwa Mkoa umekumbwa na ukame hivyo uwezekano wa kutokuwa na chakula cha kutosha kwa mwaka huu upo.

**AZIMIO NA.6:** Viongozi katika ngazi ya Wilaya (mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri) walishauriwa kwenda kuhamasiha wananchi kulima mazao yanayostahimili ukame na yanayokomaa haraka Mfano: Mbogamboga, na mazao ya Mikunde. Aidha, walishauriwa kwenda kusisitiza na kusimamia kila kaya kununua na kuweka akiba ya kutosheleza mahitaji ya kaya kwa mwaka mzima.

## AGENDA NA. 10: MUHT NA. 10: MAENDELEO YA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI:

**HOJA NA. 6:** Katika agenda hii, wajumbe walisema baadhi ya dawa za Chanjo hazipatikani na Mkoa wetu una magonjwa mengi kwa mifugo

ukizingatia kuwa tuko mpakani na nchi jirani na mifugo imekuwa ikiingia na kutoka kutoka nchi hizo.

**AZIMIO NA. 7:** Kila Halmashauri iweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa dawa halisi za mifugo zinapatikana kwa wakati na za kutosha.

## AGENDA NA. 11: MUHT. NA. 11: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO 2015/2016:

Taarifa ya utekelezaji ilisomwa na wajumbe waliipitisha.

## AGENDA NA 12: MUHT. NA. 12: MADA MAALUMU

Agenda hii haikuwasilishwa.

## AGENDA NA. 13: MUHT. NA. 13: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Katika mengineyo Mwenyekiti alimwagiza Katibu Tawala wa Mkoa yafuatayo:-

(i) Kuandaa mafunzo mafupi kwa ajili ya Viongozi wote wa Mkoa ili kila mmoja aweze kujua majukumu na mipaka yake ya kazi ili kuweza kuleta ufanisi na kuondoa migongano isiyo na sababu.

(ii) Afisa kutoka Ofisi ya Maadili Viongozi wa Umma aliwakumbusha Viongozi wa Umma kuwasilisha tamko la mali na madeni kabla ya tarehe 30 Desemba kila mwaka na kupeleka Ofisi ya Kamishna wa maadili Kanda ya Arusha.

(iii) Vilevile wajumbe walikumbushwa kuwa kikao cha RCC kiwe ni kikao cha kushauri zaidi kuliko malalamiko. Kwani ilionekana kuwa tokea mwanzo malalamiko ndiyo mengi kuliko ushauri.

(iv) Wajumbe walipendekeza suala la shule za Sekondari kuungua moto liangaliwe kwa kina kwani si kitu cha kawaida.

(v) Wajumbe walikumbushwa suala la uadilifu hasa wanapokuwa kwenye vikao.

**AGENDA NA. 14: MUHT. NA. 14: KUFUNGA KIKAO:**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 12.30 jioni kwa kuwataka wajumbe kukubaliana na mabadiliko yaliyopo na wajifunze kusoma alama za nyakati, na kwenda na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano. Vile vile aliwataka wajumbe kwenda kusimamia ukusanyaji mapato na matumizi ya Halmashauri zao. Mwisho kabisa aliwataka wajumbe kujenga Ushirikiano, Mshikamano na Umoja ili kujenga Mkoa wa Arusha na kutatua kero za wananchi.

**Muhtasari Umethibitishwa**

________________________ Mwenyekiti

________________________ Katibu

________________________ Tarehe

**UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA USHAURI YA MKOA (REGIONAL CONSULTATIVE COMMITTEE (RCC) KILICHOFANYIKA TAREHE 21/10/2016 KATIKA UKUMBI WA MKUU WA MKOA WA ARUSHA**

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Taarifa zilizotolewa nyingi hazikuwa sahihi na takwimu zake zilitiliwa mashaka na kamati | 1. Kamati ilipendekeza kuwa katika kutoa taarifa za utekelezaji wa maazimio kikao kijacho kila Halmashauri itatoa taarifa yake wenyewe kwa kufuata fomati ambayo itaelekezwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa | Mh. RC<br>Wah. DC<br>Wakurugenzi wa Halmashauri | **1. JIJI LA ARUSHA**<br>Agizo litazingatiwa. Halmashauri ya Jiji la Arusha itatumia fomati ambayo itaelekezwa katika kuwasilisha taarifa. |
| | | | | **2. HALMASHAURI YA WILAYA YA KARATU**<br>Agizo limezingatiwa kuanzia taarifa za kikao kijacho, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu itahakiki taarifa zake kabla ya kuziwasilisha katika kikao ili kuepuka kuwasilisha taarifa zenye takwimu zisizo sahihi |
| | | | | **3. HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**<br>Taarifa nyingi ikihusisha Takwimu mbalimbali zinazowasilishwa Mkoani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, kwa kawaida huanza kuandaliwa kutoka kwenye Idara husika na wakuu wa Idara wameagizwa kuhakikisha kuwa wanajiridhisha na Takwimu au taarifa yao kabla ya kuiwasilisha kwa timu inayohusika kukusanya Takwimu au Taarifa zote kutoka Idara mbalimbali na kuzifanyia uhakiki wa |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kikao. Hii ni kutokana na taarifa zinazotumwa Mkoani baadhi kuonekana hazina ukweli ndani yake wala hazina takwimu za kutosha. | | Taarifa au Takwimu hizo kabla ya kuziwasilisha Mkoani, Lengo la utaratibu huu ni ili kuhakikisha kuwa Taarifa yoyote au Takwimu zozote kutoka Halmashauri ya Monduli zinakuwa sahihi. |
| | | | | **4. HALMASHAURI YA WILAYA MERU**<br>Taarifa hii itawasilishwa na RMO |
| | | | | **5. HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**<br>Agizo limezingatiwa, tunasubiri maelekezo ya Mkoa. |
| | | | | **6. HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**<br>Mfumo wa ukusanyaji na utunzaji wa takwimu umeboreshwa katika Idara zote na kanzi data *(data base)* ya Wilaya imeimarishwa ili kuwa na chanzo kimoja cha taarifa. |
| 2. | Taarifa ya Sekta ya Afya iliyotolewa ilieleza mazuri tu bila kuleta changamoto ambazo | 2. Wajumbe walitaka taarifa ya Afya iboreshwe zaidi kwa kuongeza | Katibu Tawala Mkoa | (i) Kuelimisha jamii juu ya mtindo bora wa maisha (life style) mfano; kula chakula bora chenye virutubisho muhimu kwa kiasi sahihi na kufanya mazeozii, kuacha sigara na kupunguza unywaji wa pombe.<br>(ii) Kuwa na mazoea ya kupima afya mara kwa mara nagalau maramoja kwa maka.<br>(iii) Kuhamasisha Halmashauri kuandaa upimaji Afya za |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | zinahitajika kujadiliwa na kuwekewa mikakati | vipengele ambavyo vimeachwa kama chanjo na magonjwa yasiyoambuki za lakini yamekuwa ni tishio kama vile Kansa, presha na Sukari hii itaisaidia kamati kuweka mikakati juu ya changamoto hizo. | | jamii angalao mara mbili kwa mawka (siku ya Afya duniani na siku ya Kisukari)<br>(iv) Kuhamasisha vituo vya kutolea huduma kuwa na tabia ya kupima magonjwa hayo na kutoa elimu kwa kila mgonjwa anayefika kupata huduma.<br>(v) Kuhamasisha Halmashauri kutenga baejti katika vituo vya katulea huduma kufanya zoezi la kupima na vihakikishe kuwe na vifaa vya kupima urefu, uzito, sukari, shinikizo la damu, saratani n.k.<br>(vi) Kuhamasisha jamii, taasisi binafsi na za Serikali kutenga siku maalum na sehemu maalum kwa ajili ya kufanya mazoezi hasa kwa wafanyakazi kazini.<br>(vii) Jeshi la polisi lisaidie kutoa elimu kwa jamii juu ya ongezeko la ajali za barbarani na jinsi gani ya kuzipunguza.<br>(viii) Watoa huduma za afya wapate mafunzo ya jinsi gani ya kutoa huduma kwa majeruhi waliopata ajali.<br>(ix) Wataalam wa Mkoa waliopata mafunzo juu ya kutoa huduma kwa majeruhi wa ajali wasaidie kufundisha wataalam wengine katika halmashauri. |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Wajumbe walisema kumekuwa na miradi mingi mno ya maji ambayo haitekelezeki, na wakandarasi wengi wameacha kazi na kuondoka eneo la mradi bila kukamilisha kazi walizopangiwa kwa mujibu wa mikataba yao. | 3. Wajumbe walipendekeza kuwepo na miradi michache ya maji ambayo nguvu ya fedha itaelekezwa huko na kuweza kukamilika kwa wakati kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haitekelezeki. | Wakurugenzi wa Halmashauri | **1. JIJI LA ARUSHA**<br>Agizo limezingatiwa. Halmashauri ya Jiji la Arusha imekabidhi Mradi wa Maji kwa AUWASA kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa mradi huu. |
| | | | | **2. HALMASHAURI YA WILAYA YA KARATU**<br><br>Azimio limezingatiwa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kwa mwaka wa fedha 2017/18 imepanga kutekeleza miradi 7 mipya na kukarabati miradi 9 kutokana na ushauri wa Wizara, Aidha katika robo ya pili ya Mwaka 2016/17, Serikali imeipatia Halmshauri ya Wilaya ya Karatu kiasi cha **Tshs. 548,236,603.02** kwa ajili ya kuendelea kulipa madeni ya wakandarasi wa Miradi ya Maji inayoendelea. |
| | | | | **3. HALMASHAURI YA WILAYA MONDULI**<br>Agizo hili limezingatiwa kwa mwaka 2016/2017, Halmashauri ya Monduli imeingia mikataba kulingana na bajeti iliyopitishwa katika kutekeleza miradi ya maji. Aidha, mikataba hii imelenga kukamilisha miradi viporo kwanza kabla ya kuanza miradi mipya. |
| | | | | **4. HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**<br>Kati ya vijiji 10, miradi katika vijiji vitatu imekamilika na miradi 7 iliyobaki, wakandarasi wake wanaendelea na kazi. |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **5. HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO**<br>Wakandarasi wamerudi sehemu ya ujenzi wa mradi na wanaendelea na ukamilishaji wa miradi baada ya kuhakikishiwa kuwa watalipwa madai yao. |
| | | | | **6. HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**<br>Agizo limezingatiwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018 imetengwa miradi michache ambayo kwa kiasi kilichotengwa itakamilika na kuepuka miradi viporo. |
| | | | | **7. HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**<br>Miradi iliyopo inatekelezeka endapo fedha zitakuja kwa wakati. |
| 4. | Afisa Elimu Mkoa akiwasilisha mada, alieleza kuwa kuhusu tatizo la madawati Ngorongoro hakuna | 4. Kamati iliazimia kuwa taarifa hizo hazikuwa sahihi, na kumwagiza Afisa Elimu wa Mkoa kuleta taarifa | Katibu Tawala Mkoa | Agizo limezingatiwa na Mkoa umerekebisha takwimu za madawati kwa shule za Msingi na Sekondari hadi kufikia tarehe 1/2/2017 kwa mchanganuo ufuatao:- |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | upungufu wa madawati, jambo ambalo wajumbe walikataa na kumwambia kuwa taarifa zake sio sahihi kwani hadi tarehe ya kikao kulikuwa na upungufu wa madawati zaidi ya 1,500. Na kuna baadhi ya shule watoto bado wanakaa chini. | sahihi za madawati katika kikao kijacho. | | **TAARIFA YA HALI YA MADAWATI KWA SHULE ZA MSINGI ZA SERIKALI** |

**SHULE ZA MSINGI**

| S/N | HALMA-SHAURI | IDADI YA SHULE ZILIZOPO | IDADI YA WANAFUNZI | MADA-WATI YANAYO-HITAJIKA | MADAWATI YALIYOPO | YANA YOTE NGEN EZWA | UPUNGU-FU WA MADA-WATI KWA SASA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **ARUSHA JIJI** | 48 | 61,447 | 20,831 | 22,058 | - | - |
| 2 | **ARUSHA DC** | 92 | 62,385 | 20,782 | 20,782 | - | - |
| 3 | **KARATU** | 105 | 49,138 | 24,569 | 25,697 | - | - |
| 4 | **LONGIDO** | 41 | 15,039 | 9,040 | 9,144 | - | - |
| 5 | **MERU** | 112 | 52,979 | 26,490 | 26,311 | - | 179 |
| 6 | **MONDULI** | 59 | 25,730 | 9,120 | 11,994 | - | - |
| 7 | **NGORO-NGORO** | 62 | 35,001 | 11,667 | 13,372 | 1,252 | - |
| | **JUMLA** | **519** | **301,719** | **122,499** | **129,358** | **1,252** | **179** |

**SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI**

| NA | HALMA-SHAURI | WANA-FUNZI | MAHITAJI | | VILIVYOPO | | PUNGUFU | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | VITI | MEZA | VITI | MEZA | VITI | MEZA |
| **1** | LONGIDO | 5,290 | 5,290 | 5,290 | 5,200 | 5,200 | 90 | 90 |
| **2** | ARUSHA DC | 18,385 | 18,385 | 18,385 | 17,294 | 17,294 | 1,091 | 1,091 |
| **3** | MERU DC | 11,889 | 11,889 | 11,889 | 11,889 | 11,889 | | |
| **4** | KARATU | 9,926 | 9,926 | 9,926 | 10,470 | 10,470 | | |

<table>
<tr><th>Na.</th><th>Hoja</th><th>Azimio</th><th>Mhusika</th><th>Utekelezaji</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td><td>
<table>
<tr><td>5</td><td>MONDULI</td><td>6,678</td><td>6,678</td><td>6,678</td><td>6,456</td><td>6,456</td><td>222</td><td>222</td></tr>
<tr><td>6</td><td>NGORONG ORO</td><td>5,312</td><td>5,312</td><td>5,330</td><td>5,678</td><td>5,678</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>7</td><td>ARUSHA CC</td><td>23,776</td><td>23,776</td><td>23,776</td><td>23,776</td><td>23,776</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>JUMLA</td><td>81,256</td><td>81,256</td><td>81,274</td><td>80,763</td><td>80,763</td><td>1,403</td><td>1,403</td></tr>
</table>
</td></tr>
<tr><td>5.</td><td>Suala la upatikanaji wa chakula cha uhakika katika Mkoa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi, kwa sehemu kubwa Mkoa umekumbwa na ukame hivyo uwezekano wa kutokuwa na chakula cha kutosha kwa</td><td>5. Viongozi katika ngazi ya Wilaya (Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri) walishauriwa kwenda kuhamasisha wananchi kulima mazao yanayostahimili ukame na yanayokomaa haraka Mfano:</td><td>Wakuu wa Wilaya<br><br>Wakurugenzi wa Halmashauri</td><td>1. JIJI LA ARUSHA<br>Wananchi kwenye maeneo wanayolima wamehamasishwa kuandaa mashamba yao mapema kwa ajili ya kilimo cha masika.<br>Kuandaa pembejeo zote muhimu<br>Kupanda kwa wakati mara tu mvua zitakapoanza kunyesha<br><br>Kupanda mazao yanayo-stahimili ukame na yanayo komaa haraka kama vile viazi vitamu, mbogamboga, mikunde, mihogo na mahindi ya muda mfupi.<br><br>Wakulima wameshauriwa kuendelea na utunzaji wa zao la mgomba<br><br>Halmashauri inafuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji wa vyakula muhimu kwenye masoko na bei ya kujiridhisha.<br><br>Wananchi wameelimishwa kujinunulia chakula na kukihifadhi</td></tr>
</table>

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | mwaka huu upo. | Mbogambog, na mazao ya Mikunde. Aidha, walishauriwa kwenda kusisitiza na kusimamia kila kaya kununua na kuweka akiba ya kutosheleza mahitaji ya kaya kwa mwaka mzima. | | kwa ajili ya matumizi ya baadaye.<br>Pia wananchi wameshauriwa kutumia vyakula vingine visivyokuwa vya nafaka na kutumia vizuri akiba ya chakula walionayo. |
| | | | | **2. HALMASHAURI YA WILAYA YA KARATU**<br>Agizo limezingatiwa Mkuu wa wilaya mwezi Novemba alitoa agizo kwa Maafisa Tarafa na watendaji wa Kata zote (14) kuhusu kuwaelekeza wananchi kutunza na kununua chakula pamoja na kulima mazao yanayostahimili ukame kama mazao jamii ya mikunde. Aidha Mkuu wa wilaya pamoja na Mkurugenzi hadi sasa wamefanya Mikutano ya hadhara pia Vikao na viongozi wa Vijiji vipatavyo 21 (Chemichemi, K/Moja, Kinihe, Basodawish, Khusumay, Kitete, Lositete, Mahaha, Getamock, Buger, Ayalaliyo, Endashangwet, Jobaj, Mang'ola barazani, Mikocheni, Laghangareri, Qaru, Changarawe, Laja, Umbagw' na Oldean) Kuhamisisha utunzaji na ununuzi wa chakula pamoja na kilimo cha mazao yanayostahili ukame na ufanisi wake utaonekana mara baada ya Msimu wa Masika wa 2016/17 unaotarajiwa kuanza Machi, 2017. Kwa upande wa bonde la Eyasi wakulima wamehamasishwa kulima Mahindi zaidi badala ya Vitunguu ili kuongeza uhakika wa Chakula. |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Kwa kipindi cha Januari, 2017 Kaya karibu zote zilikuwa na \chakula cha kutosha kwani ilibainika kuna tani 500 za Mahindi kwenye Maghala ya Vijiji kumi na sita (16) |
| | | | | **3. HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**<br><br>Katika kutekeleza agizo hili, uhamasishaji na ushauri juu ya kulima mazao yanayostahimili ukame na kukomaa kwa muda mfupi umetolewa katika vikao vyote vya hadhara vilivyofanyika vijijini, Watendaji wa kata na vijiji, na katika vikao vikuu vya Halmashauri wakati wa bajeti Januri, 2017 kamati za madiwani na Baraza kwa ujumla ili msisitizo uweze kufanyika kwa wanachi kutekeleza kwa vitendo katika Wilaya nzima,Pia msisitizo zaidi umeendelea kutolewa, Mvua zilizoanza mwanzoni mwa mwezi Februari, 2017 zimetumika kwa wakulima kupanda mahindi kwa msukumo mkubwa, mbegu ya DK (DEKALD) inayokomaa kwa muda muda mfupi na yenye uwezo wa kustahimili Ukame. |
| | | | | **4. HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**<br>Wakulima wamehamasishwa kupitia mikutano ya vijiji na Kamati za Maendeleo za Kata kulima mazao yanayostahili ukame ambayo mihogo, mtama, mbaazi na viazi vitamu. |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **5. HALMASHAURI YA WILAYA LONGIDO**<br>Wilaya ina Mkakati wa kuhamasisha wafugaji kuuza mifugo yao na kujinunulia chakula na kuhifadhi kwa ajili ya matumizi ya baadae pia wakulima wanaendelea kushauriwa kulima mazao ya muda mfupi kama vile Njegere, Mahindi (Chotara) yanayokomaa kwa muda mfupi kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo kama IIED Kuibuwa miradi inayoweza kusaidia upatikanaji wa chakula na uhakika wake kama vile kilimocha Mtama na Mihogo. |
| | | | | **6. HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**<br>Agizo limezingatiwa elimu na uhamasishaji umeendelea kutolewa na maafisa ugani na maendeleo ya jamii waliopo katika Kata na Vijiji. |
| | | | | **7. HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**<br>Maafisa Ugani Vijijini wameendelea kuwahamasisha wakulima kulima mazao yanayokomaa haraka. Pia maeneo ya umwagiliaji wakulima wanatumia vema kilimo cha umwagiliaji. |
| 6. | Baadhi ya dawa za Chanjo hazipatikani na | 6. Kila Halmashauri iweke utaratibu | Wakuu wa Wilaya<br><br>Wakurugenz | **1. JIJI LA ARUSHA**<br>Agizo limezingatiwa. Utaratibu wa kuwa na chanjo umeandaliwa na kuingizwa kwenye bajeti ya 2017/2018, chanjo hizo ni Kimeta, Kichaa cha mbwa na Kideri. |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | Mkoa wetu una magonjwa mengi kwa mifugo ukizingatia kuwa tuko mpakani na nchi jirani na mifugo imekuwa ikiingia na kutoka kutoka nchi hizo. | mzuri wa kuhakikisha kuwa dawa halisi za mifugo zinapatikana kwa wakati na za kutosha. | i wa Halmashauri | **2. HALMASHAURI YA WILAYA YA KARATU** Halmashuari ya Wilaya ya Karatu ina maduka 19 ya kuuza dawa za Mifugo yaliyosajiliwa na yanakaguliwa mara moja baada miaezi mitatu (robo mwaka) ili kuhakikisha kuwa dawa zilizopo ni salama na zimeruhusiwa kwa matumizi ya Mifugo ndani ya nchi. Aidha ukaguzi wa robo ya pili (Oktoba – Desemba, 2016) ulifanyika na lita 120 za dawa za minyoo ambazo hazikuwa zimesajiliwa zilikamatwa na kuharibiwa |
| | | | | **3. HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI** Halmashauri imefanya kikao na wadau wa pembejeo za mifugo mnamo tarehe 18-01-2017 Eneo la mesereani na kukubaliana kuingiza madawa (chanjo na Tiba) ya Mifugo halisi na yakutosha kwa wakati. Pia Halmashauri ya Wilaya Monduli, imejipanga kununua chanjo za magonjwa ya mlipuko dozi **25,000** kutoka Maabara kuu ya Taifa ya Serikali ya magonjwa ya Mifugo Temeke. Hata hivyo, Halmashauri inaendelea kutoa Elimu kwa wafugaji Juu ya kuchanja mifugo wakati ikiwa na afya na kwa wakati. |
| | | | | **4. HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU** Halmashauri imeweka utaratibu wa kununua chanjo kwa pamoja na kuzigawa kwa wataalam wa mifugo wa Kata. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2016/17, Halmashauri |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | | imenunua chanjo ya kimeta yenye thamani ya Tsh. 9,600,000/=. Ili kudhibiti uhalisia wa madawa chanjo hizi zilinunuliwa kutoka kwa Wakala wa maabara ya Veterinary. |
| | | | | **5. HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO**<br>Dawa za chanjo zinazotumika zimeidhinishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria na mahitaji ya chanjo yanapajitokeza mawasiliano yanafanyika wizarani kuhusiana na aina ya chanjo zinazohitajika<br><br>Pia ukaguzi wa mara kwa mara unafanyika kwenye maduka ya madawa ili kuona ubora kwa kushirikiana na mamlaka ya chakula na Dawa (TFDA) kanda. |
| | | | | **6. HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**<br><br>Upatikanaji wa chanjo halisi na kwa wakati katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha unasimamiwa na Idara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na TVLA.<br><br>Chanjo hizo ni za magonjwa ya kimeta (Anthrax) na Ndondo (Newcastle) ambazo hutengenezwa na kusambazwa na TVLA. |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Idara ya Mifugo na Uvuvi, pia inahakikisha/inasimamia chanjo za magonjwa mengine kama kichaa cha mbwa zinapatikana kwa wakati na kutoka vyanzo vinavyoeleweka. |
| | | | | **7. HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO** Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetenga shilingili 204,000,000/= kwa ajili ya gharama za manunuzi ya chanjo mbalimbali katika mchanganuo ufuatao; ECF 30,000,000/= ATHRAX 25,000,000/= PPR/CCPP/CBPP 149,000,000/= katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa sababu uingizaji wa chanjo za PPR/CCPP/CBPP ni lazima upitie Wizara ya Mifugo na uvuvi. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imewaandikia barua Wizara ili kupata kibali cha uingizaji wa chanjo hizo. Halmashauri ya Wilaya imetenga TSh.10,000,000/= kwa ajili ya kuingiza chanjo ya CBPP/PPR katika mwaka wa fedha 2016/2017. Pia katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Idara inategemea kuwasilisha makisio ya TSh.50,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa chanjo. Fedha hizi zitatengwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (LDF), mfuko utakao kuwa ukijiendesha kwa wafugaji kuchangia gharama za kuchanja, hivyo basi mfuko unategemewa kuongezeka kila mwaka na kufanya huduma hii kuwa endelevu. |

| Na. | Hoja | Azimio | Mhusika | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Baadhi ya Viongozi kuto kujua mipaka ya majukumu yao. | 7. Kuandaa mafunzo mafupi kwa ajili ya viongozi wote wa Mkoa. | Katibu Tawala Mkoa | Viongozi watapewa maelekezo katika kikoa maalum kitakachofanyika tarehe 16/2/2017 kuhusu maadili ya viongozi |

# PRESENTATION
# 26-39

## KIAMBATANISHO 1

## MCHANGANUO WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 (MID YEAR REVIEW)

## SEKRETARIET YA MKOA

| SEKTA | LENGO LA MRADI KWA MWAKA | UTEKELEZAJI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| UTUMISHI NA UTAWALA | Kuhakikisha vikao na ziara za viongozi ngazi ya Mkoa vinafanyika ifikapo Juni 2018 | Ziara 12 za viongozi ngazi ya Mkoa zimefanyika katika Wilaya | **68.5** |
| | Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi 144 ifikapo Juni 2019 | Upatikanaji wa vifaa vya kutendea kazi na fanicha zimetolewa kwa watumishi 116<br>- Shughuli za itifaki zimewezeshwa katika ngazi ya MNkoa<br>- Taarifa mbalimbali za utendaji kazi na maagizo ya serikali zimetolewa kwa watumishi, ikiwemo zoezi la kuhakiki vyeti, kulipa madeni ya watumishi na kuandaa bajeti za Halmashauri na Mkoa pamoja na bajeti za mishahara | **59** |
| | Kuandaa na kushiriki katika sherehe za Kitaifa na Kimataifa na | Kikao kimoja cha baraza la wafanyakazi kimefanyika | **50** |

| SEKTA | LENGO LA MRADI KWA MWAKA | UTEKELEZAJI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | kufanya vikao vya kisheria vya Baraza la wafanyakazi ifikapo Juni 2018 | tarehe 15/2/2016 | |
| | Kutoa mafunzo na elimu kwa watumishi 115 juu ya kutekeleza wajibu katika maeneo ya kazi | Watumishi 15 wamepata mafunzo juu ya masuala ya utumishi na kusimamia shughuli za maendeleo kwenye Halmashauri | **26** |
| **FEDHA** | Kuhakikisha mishahara na stahiki za watumishi zinalipwa ifikapo Juni 2018 | Malipo ya mishahara kwa watumishi 450 na madai mengine yamelipwa kwa awamu na zoezi linaendelea | 45 |
| | Kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi kwa watumishi 14 ifikapo Juni 2018 | Mazingira pamoja na vitendea kazi kwa watumishi 14 yameboreshwa | **56** |
| | Kuimarisha kitengo cha fedha na kuhakikisha kinaimarika ifikapo Juni 2019 | Utendaji kazi wa kitengo cha fedha kimeimarishwa | |
| **MKAGUZI WA NDANI** | Kuboresha huduma za watumishi katika kitengo cha ukaguzi | Bado taratibu za kununua vifaa vya kutendea kazi unaendelea | |
| | Kufanya ukaguzi wa kila robo ya mwaka wa matumizi ya fedha za serikali ifikapo Juni | Ukaguzi umefanyika na Taarifa ya ukaguzi robo ya nne 2015/2016 imewasilishwa kwa | 50 |

| SEKTA | LENGO LA MRADI KWA MWAKA | UTEKELEZAJI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | 2018 | utekelezaji | |
| **KITENGO CHA MANUNUZI** | Kuhakikisha mazingira ya kazi yanaboreshwa kwa watumishi 4 wa kitengo cha ugavi | | |
| | Kuhakikisha Sekretariet ya Mkoa inakuwa na Mpango kazi wa manunuzi na kufanya manunuzi ifikapo Juni 2017 | Shughuli za manunuzi ya serikali zimekuwa zikiendelea kila wakati kulingana na mpango kazi pamoja na upatikanaji wa fedha | **50** |
| **MIPANGO NA URATIBU** | Kusimamia na kukagua mipango na bajeti za mkoa na halmashauri ifikapo Juni 2018 | Kazi ya kupitia na kuratibu bajeti na mipango za sekretariet na halmashauri zimefanyika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/2017 | 50 |
| | Kuhakikisha stahiki za kisheria za watumishi wa seksheni zimelipwa ifikapo Juni 2017 | Malipo ya posho za kisheria na posho zingine zimelipwa | 50 |
| | Kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri zote saba | Ukaguzi wa miradi ya maendeleo haujafanyika kwa robo mbili, baada ya fedha kuchelewa kutolewa na serikali | 0 |
| UCHUMI NA UZALISHAJ | Kuwezesha wataalam 19 kufanya shughuli za ushauri katika Halmashauri zote 7 | Watumishi 19 walishiriki katika mikutano ya kitaaluma na sherehe za Nane nane pamoja na | 59 |

| SEKTA | LENGO LA MRADI KWA MWAKA | UTEKELEZAJI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| I | kwenye sekta za kilimo, mifugo, viwanda, biashara na utalii | Sabasaba | |
| | Wataalam 5 kushiriki katika kufanya tathmini ya mifugo na kuboresha mifugo hiyo kwa kufanya uhamilishaji(artificial inermination) pamoja na kukinga mifugo dhidi ya magonjwa ya mifugo | Wataalam 5 wameshiriki katika shughuli za kufanya tathmini na kutoa chanjo ya mifugo katika Halmashauri<br>- Watumishi 2 walishiriki katika kufanya tathmini ya mabwawa ya samaki na kuangalia uzalishaji pamoja na kukataza uvunaji haramu wa samaki | 73.3 |
| MIUNDO MBINU | Kuhakikisha vikao vya kisheria vya Barabara vinaitishwa kwa wakati kila robo ya utekelezaji | Kikao kimoja cha Barabara kimeitishwa mwezi wa Novemba 2016 | 53 |

**Changamoto zinazoikabili sekcretariet ya mkoa katika kutekeleza majukumu yake**

1. Kuchelewa kutolewa kwa wakati kwa fedha za miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo ambapo hali hii imezifanya idara za mkoa kushindwa kutekeleza shughuli zake kwa wakati, mfano ukaguzi wa miradi, ufafanuzi wa sera mbalimbali za kitaifa, n.k

2. Kuwepo kwa mawasiliano duni kati ya Mkoa na Halmashauri zilizopo pembezoni mwa Mkoa, hali inayopelekea ucheleweshaji wa kupeleka na kupokea taarifa kwa ajili ya utekelezaji.

3. Kubadilika mara kwa mara kwa maagizo ya serikali kuhusu baadhi ya sheria za kuendesha shughuli za serikali za Mitaa, mfano suala ya property tax ambalo kwa kiasi kikubwa lilichangia Halmashauri zenye maeneo ya ukusanyaji huo kushindwa kufikia malengo.

4. Maelekezo mengi yanayotolewa na serikali kupitia Wizara mbalimbali zenye sekta zake katika Mkoa ambazo wakati mwingine maagizo hayo yanahusisha fedha ambazo hazipo katika bajeti, mfano usimamizi wa mitihani ya darasa la saba, nne na sekondari..

5. Uhaba wa watumishi katika baadhi ya seksheni na vitengo, ambapo kwa mda mrefu serikali haijatoa vibali vya ajira vya kada hizo

**TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATIKA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA KUANZIA JULAI HADI DESEMBA 2016-**

**HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA**

| SEKTA/ PROGRAMU | JINA LA MRADI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| AFYA | Kukamilisha ujenzi wa zahanati 5 na vituo vya afya 3 ifikapo Juni 2017 | Zahanati 1 imejengwa katika Kata ya Elerai na kukamilika, Zahanati za Kimandolu na Baraa zinaendelea kujengwa. i | 30 |
| UTAWALA | Kujenga ofisi za Kata 3 ifikapo Juni 2017 | Ujenzi wa ofisi moja ya Kata umefanyika (katika kata ya Kati) ujenzi wa ofisi nyingine 2 unaendelea | 25 |
| ELIMU MSINGI | Kujenga vyumba vya madarasa 56 katika shule za msingi ifikapo Juni 2017 | Ujnzi wa vyumba vya madarasa 56 unaendelea na kazi imefikia katika hatua nzuri | 70 |

| SEKTA/ PROGRAMU | JINA LA MRADI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| ELIMU SEKONDARI | Kujenga vyumba vya madarasa 25 katika shule za sekondari ifikapo Juni 2017 | Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari 25 unaendelea | 50 |
| MAENDELEO YA JAMII | Kuwawezesha akina mama na vijana katika kujikwamua kiuchumi | Kiasi cha Tshs 589,830,539 zimetolewa kwa vikundi vya akina mama na vijana | 30 |
| | Kupunguza maambukizi ya UKIMWI kwa wale wanaoishi katika mazingira magumu kutoka asilimia 12 hadi 7 ifikapo Juni 2016 | Shughuli hizi bado hazijafanyika kutokana na kuchelewa kutolewa kwa fedha | 0 |
| ARDHI NA MIPANGO MIJI | Kupima na kupanga maeneo 6 ya Jiji kwaajili ya makazi ifikapo Juni 2016 | Kazi haijafanyika kutokana na kazi ya kutengeneza Master Plan ya Jiji | |
| | Kufanya tathmini ya majengo na nyumba zipatazo 15,000 kwa ajili ya kukadiria mapato ya majengo (property Tax) | Jumla ya majengo 18,000 yameshafanyiwa tathmini | 120 |
| BARABARA | Kuhakikisha jumla ya Km 164.5 za barabara za changarawe zinakarabatiwa pamoja na Km 15 za barabara kufanyiwa matengenezo makubwa pamoja na kuzikarabati. Pia | Km 48 za barabara za changarawe zimekarabatiwa, Km 32 za barabara ya lami zimejengwa | 38 |

| SEKTA/ PROGRAMU | JINA LA MRADI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | kufungua Km 10 za barabara za Mjini na Km 72 za barabara kuwekwa lami ifikapo Juni 2017 | | |
| FEDHA NA BIASHARA | Kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha kila mwezi | Ukaguzi umefanyika mara 6 katika eneo la matumizi ya fedha na ubora wa kazi | 50 |
| | Kuandaa ripoti 12 za ukaguzi za kila robo ya mwaka ifikapo Juni 2017 | Mpaka sasa ripoti 2 zimeshaandaliwa | 16 |
| | Kuhakikisha mapato ya ndani yanaongezeka kutoka Tshs 13 Bilioni hadi Tshs 17 Bilioni ifikapo 2017 | Mpaka sasa kiasi cha Tshs 7,807,034,772.52 zimekusanywa kati ya Tshs 17 Bilioni zilizokadiriwa kukusanywa | 45 |
| UTAWALA | Kuhakikisha watumishi 254 kati ya watumishi 323 wanafikiwa na huduma na kuboreshewa mazingira mazuri ya kutenda kazi kila wakati hadi ifikapo mwaka 2017 | Watumishi wanapatiwa huduma zote za kisheria ikiwemo kulipwa mishahara na stahiki zingine | 80 |
| | Kuhakikisha kiwango cha vikao vya kisheria kinapanda na kufikia vikao 40 ifikapo Juni 2017 | Vikao 12 vya kisheria vimeketi | 30 |

| SEKTA/ PROGRAMU | JINA LA MRADI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | Kushiriki katika sherehe zote za Kitaifa ifikapo Juni 2017 | Sherehe zote za kitaifa kwa miezi sita iliyokwisha zimewezeshwa | 50 |
| | Kuhakikisha kunakuweko na Amani na Utulivu katika maeneo yote ya Jiji ifikapo Juni 2017 | Amani na utawala bora vimedumishwa katika Kata zote 25 kwa kipindi cha miezi 6 iliyopita | 100 |
| | Kushughulikia na kutatua migogoro mbalimbali kutoka 27 iliyopo hadi 9 ifikapo Juni 2017 | Mgogoro mmoja kati ya 27 umetatuliwa | 10 |
| SERA NA MIPANGO | Kuhakikisha Halmashauri inachangia asilimia 60 katika miradi ya maendeleo ifikapo Juni 2017 | Jumla ya Tshs 3.5 Bilioni kati ya Tshs 10.7 Bilioni zimeshatolewa na kuchangia miradi ya maendeleo | 50 |
| | Kuhakikisha miradi 90 ya maendeleo katika Kata na Mitaa inakaguliwa na kufanyiwa tathmini ifikapo Juni 2017 | Jumla ya miradi 70 imeshagaguliwa na kufanyiwa tathmini katika utekelezaji wake | 50 |
| | Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi kila robo ya mwaka ifikapo Juni 2017 | Ripoti 2 za taarifa ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo zimeandaliwa na kuwasilishwa | 50 |

| SEKTA/ PROGRAMU | JINA LA MRADI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| ARDHI UTAWALA | Kuhakikisha kunakuweko na Upimaji wa viwanja 3,000 vya makazi na huduma za kibiashara katika Kata zote 25 ifikapo Juni 2017 | Kazi hizi hazijaanza na zinatarajiwa kuanza katika robo ya tatu | 0 |
| | Kufanya savei ya barabara mpya katika mitaa na kata Km 15 ifikapo Juni 2017 | Kazi hii itatekelezwa katika robo ya 3 na 4 ya mwaka huu wa fedha | 0 |
| | Kuhakikisha viwanja 1,500 vinapimwa | Kazi haijafanyika | 0 |
| MALIASILI NA MAZINGIRA | Kuanzisha maeneo mapya ya Utalii (Eco-tourism) ifikapo Juni 2017 | Kazi hii haijaanza, na inatarajiwa kuanza robo ya 3 na 4 ya utekelezaji | 0 |

**Changamoto zinazoikabili Halmashauri katika kutekeleza shughuli za Maendeleo**

1. Kucheleweshwa kwa fedha kutoka serikalini na wafadhili wengine, ambako kumesababisha ucheleweshaji mkubwa wa kutekeleza miradi kwa wakati
2. Ugumu na uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi katika kulipa ushuru mbalimbali na kodi imesababisha Halmashauri kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani.
3. Fedha chache zinazotolewa na serikali ukilinganisha na mahitaji muhimu ya wananchi yanayohusu maendeleo na huduma bora kwa jamii

**Mikakati ya kukabiliana na changamoto kwa siku za mbele**

1. Kuwaelimisha wananchi juu ya kutoa michango yao kwenye kazi za maendeleo
2. Kuwa na mpango mkakati kati ya wataalam na wananchi katika kusimamia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa pamoja
3. Kuwapata wataalam washauri wa masuala ya uwekezaji mfano ujenzi wa kituo kikubwa cha mabasi Moshono na kuhakikisha mikakati yote iliyowekwa ya kukusanya mapato ya ndani inatekelezeka ili kuweza kuendesha miradi mikubwa kama huu

**HALMASHAURI YA KARATU**

| SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| AFYA | Kuhakikisha Halmashauri inatenga asilimia 60 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kuongeza kiwango kufikia asilimia 80 ifikapo Juni 2019 | Asilimia 60 ya kuchangia miradi ya maendeleo imefanyika | 86 |
| | Kupunguza upungufu wa nyumba za watumishi wa Afya katika zahanati na vituo vya afya ngazi zote ifikapo Juni 2019 | Kazi ya maandalizi ya manunuzi imefanyika kwa asilimia 20 , fedha mpaka sasa hazijapokelewa | 20 |
| MIFUGO | Kuongeza huduma na miundombinu ya mifugo kutoka asilimia 60 ya sasa hadi asilimia 70 ifikapo Juni 2019 | Miradi miwili ya kuboresha huduma za mifugo ipo katika hatua za manunuzi kwa asilimia 20 | 20 |
| | Kuhakikisha huduma za mifugo zinaboreshwa ili | Kazi za manunuzi zimefanyika kwa | 10 |

| SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | kuwa na mifugo bora yenye kuleta tija kutoka asilimia 70 hadi 80 ifikapo Juni 2019 | asilimia 10 | |
| KILIMO | Kuhakikisha kunakuwepo mazingira mazuri ya kuwawezesha wataalam 45 wa ugani ifikapo Juni 2019 | Watalam wa ugani wamewezeshwa na kuboreshewa mazingira ya kufanyia kazi kwa asilimia 33, kiwango ni kidogo kutokana na ufinyu wa bajeti | 33 |
| | Kuongeza kiwango cha uzalishaji mahindi kutoka ekari tani 2.5 kwa ekari hadi tani 5 ifikapo Juni 2019 | Kazi ya kuongeza kiwango cha uzalishaji imefanyika kwa asilimia 88, Halmashauri imenunua trekta la kuwasaidia wakulima kuongeza maeneo ya kilimo | 88 |
| MFUKO WA JIMBO | Kuweka umeme katika shule ya sekondari Baray ifikapo Juni 2016 | Kazi ya kuweka umeme imekamilika kwa asilimia 100 | 100 |
| MAJI (Programu ya RWSSP) | Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa wadau wa maji ifikapo Juni 2019 | Kazi hii imefanyika kwa asilimia 37 kutokana na ufinyu wa bajeti | 37 |
| | Kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa kuongeza kiwango cha huduma kutoka watu 165,000 hadi 210,000 | Miradi 5 ya maji ipo katika hatua za kukamilika pindi fedha zote zitatolewa kwa wakati | 95 |

| SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | ifikapo Juni 2019 | | |
| ELIMU SEKONDARI | Kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia kwa shule za sekondari pamoja na kulipa maslahi ya waalimu na watumishi wa Sekondari ifikapo Juni 2021 | Uboreshaji wa huduma na mazingira ya kujifunza na kufundishia kwa shule za sekondari umefanyika kwa asilimia 30, hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti | 30 |
| | Kuhakikisha fedha za capitation zinatolewa kwa wanafunzi wote 11,827 ifikapo Juni 2021 | Asilimia 76 ya fedha za capitation zimeshapokelewa kwaajili ya wanafunzi wa sekondari kulingana na bajeti na matumizi yake yamefanyika kulingana na mwongozo wa serikali | 76 |
| | Kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia kwa shule zote 29 za sekondari ifikapo Juni 2019 | Mazingira ya kujifunza na kufundishia yameboreshwa kwa asilimia 32, bado kunahitajika jitihada zaidi za kuhakikisha mazingira yanaboreshwa kwa kujenga vyumba vya darasa, vyoo na nyumba za walimu | 32 |
| | Kuhakikisha mazingira na stahiki za walimu wa | Mazingira ya kufundishia na maslahi | |

| SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | sekondari 634 yanaboreshwa ikiwemo kujenga nyumba za walimu pamoja na kulipa stahiki zao ifikapo Juni 2019 | ya walimu 634 wa sekondari yameboreshwa kwa asilimia 59 | 59 |
| UTAWALA | Kuhakikisha mazingira ya kazi yanaboreshwa kwa watumishi waliopo makao makuu ya wilaya ifikapo Juni 2019 | Mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa makao makuu yameboreshwa kwa asilimia 46 | 46 |
| OWN SOURCE | Kuhakikisha asilimia 60 inatolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka asilimia 45 ya sasa ifikapo Juni 2017 | Kuendelea kuweka mikakati ya kukusanya mapato ya ndani na kuchangia asilimia 60 katika miradi. Hadi Desemba asilimia 32 ya mapato ya ndani imetolewa katika kuchangia miradi | 32 |
| | Kuwezesha vikundi vya akina mama na vijana kwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ifikapo Juni 2019 | Asilimia 5 ya mapato ya ndani imetolewa kwaajili ya kuwawezesha akina mama na vijana kwa kipindi cha miezi 6 | 5 |
| | Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa wakuu wa idara na watumishi wengine waliopo makao makuu ifikapo Juni | Uboreshaji wa huduma na mazingira ya kufanyia kazi yameborshwa kwa | 56 |

| SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | 2021 | asilimia 56 | |
| MIRADI YA LGCDG | Kuhakikisha kunakuwepo na Mpango Mkakati wa Wilaya (strategic Plan) ifikapo Juni 2017 | Maandalizi ya kuandaa mpango mkakati yameanza kwa kutafuta mtaalam mshauri, pindi fedha itakapopatikana kutoka katika mapato ya Halmashauri kazi itaanza | 10 |
| | Kuhakikisha miradi yote inayopata fedha za LGCDG inatekelezwa kwa asilimia 100 | Fedha zimechelewa kufika, hadi sasa asilimia 10 ya fedha zilizopokelewa Desemba zimepelekwa kwenye miradi na shughuli za manunuzi zinaendelea | 10 |
| MIRADI YA MFUKO WA JIMBO | Kutekeleza kwa asilimia 100 miradi inayopata fedha za mfuko wa Jimbo | Fedha zimepokelewa lakini bado hazijapelekwa kwenye miradi husika | 0 |
| MFUKO WA BARABARA ( Benki ya Dunia) | Kujenga Km 198.3 za mtandao wa barabara ifikapo Juni 2019 | Kazi zimefanyika kwa asilimia 40 | 40 |
| MAJI | Kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama pamoja na kutunza mazingira na afya ya Jamii | Kazi za usafi wa mazingira, upatikanaji wa maji safi na salama katika mji wa Karatu umeboreshwa kwa | 65 |

| SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | kununua vifaa muhimu vya usafi na ujenzi wa vyoo 80 | |
| ARDHI | Kakamilisha upimaji wa eneo la makazi na biashara la mji wa Karatu ifikapo Juni 2019 | Kazi ya kutenga maeneo inaendelea na hadi sasa viwanja 1000 vimepimwa na barabara mpya 42 zimefunguliwa | 63 |
| | Kuhakikisha wananchi wanapatiwa elimu juu ya kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji na miji ifikapo Juni 2019 | Kazi zilizofanyika ni kutathmini mali za wananchi ambao maeneo yao yalikuwa hayajapimwa na hayajafuata taratibu za matumizi bora ya ardhi | 100 |

**Changamoto katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo**

1. Kucheleweshwa kwa fedha za miradi ambazo zimesababisha baadhi ya vifaa kupanda bei kuliko kiasi kilichokadiriwa, na kupelekea miraadi kutokamilika.
2. Ugumu miongoni mwa wananchi kutopenda kulipa kodi mbalimbali za Halmashauri hivyo kusababisha mchango wa Halmashauri katika miradi kutototolewa kwa wakati.
3. Sheria zilizopitwa na wakati au matumizi mabaya ya utumiaji wa sheria ndogo za Halmashauri ambapo imeplekea ugumu katika kukusanya mapato ya ndani.
4. Uwezo mdogo wa baadhi ya watumishi wa kada za chini katika kufanya tathmini ya miradi ya maendeleo.

5. Ufinyu wa bajeti ya kuwawezesha watu au makundi yenye mahitaji maalum pamoja na miradi midogomidogo isiyo rasmi katika maeneo ya vijiji na Kata ambayo wananchi wake hawana mitaji

**Mipango Mikakati ya kutatua changamoto hizo kwa siku za mbele**

1. Kuhakikisha kunakuwepo na ufuatiliaji wa karibu wa upatikanaji wa fedha kutoka serikali kuu na wafadhili wengine wanaochangia maendeleo.
2. Kuendelea kutoa elimu kwa walipa kodi juu ya umuhimu wa wao kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya Halmashauri yao na Nchi kwa ujumla, pia kuwa na takwimu sahihi za walipa kodi.
3. Kufuatilia kwa karibu marekebisho ya sheria ndogo za Halmashauri na kuhakikisha wananchi wana uwelewa wa sheria hizo, ili kuweza kuwapa nafasi wakusanyaji wa mapato ya Halmashauri kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.
4. Kuhakikisha kwamba kunakuwepo na ushirikishwaji wa hali ya juu wa wananchi katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
5. Kuimarisha na kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na pia kuhakikisha fedha zinapatikana kutoka kwa wachangiaji wengine wa maendeleo

**HALMASHAURI YA NGORONGORO**

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| UTUMISHI | Kuandaa sera ya kukabiliana na majanga katika Halmashauri | Sera ya kujikinga na majanga (risk management policy) | 30 |
| USAFI WA MAZINGIRA | Kuhakikisha vijiji 72 vinaendelea na miradi ya usafi wa mazingira na maji | Vijiji vyote 72 vimepata elimu juu ya usafi wa mazingira na kutumia vyoo salama, pia mradi | 20 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | safi na salama ifikapo 2017 | wa ujenzi wa dampo upo katika hatua za awali | |
| UTAWALA | Kuhakikisha na kuwashirikisha wananchi katika kuibua vipaumbele vya miradi yao ya maendeleo katika Kata 21 na Vijiji 56 ifikapo Juni 2017 | Jumla ya Serikaliz za Vijiji 18 zimepata mafunzo juu ya utawala bora na kuzingatia utawala wa sheria | 32 |
| MFUKO WA JIMBO | Kukamilisha ujenzi wa miradi mbalimbali ya wananchi inayopata fedha za mfuko wa jimbo katika Kata 28 ifikapo Juni 2017 | Ujenzi wa miradi hiyo unaendelea | 50 |
| TAKWIMU | Kuhakikisha kunakuwepo kwa takwimu sahihi za sekta mbalimbali kwa kutumia mfumo wa LGDMD/GDP katika vijiji 56 | Kazi haijaanza kwani fedha hazijapokelewa | 0 |
| FEDHA | Kuhakikisha kiwango cha kukusanya mapato | Kiasi cha Tshs 893,482,069 kimekusanywa kati ya | 45 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | ya Halmashauri kinapanda na kufikia Tshs 1,998,591,000 | makisio ya Tshs 1,998,591,000 | |
| ELIMU MSINGI | Kuboresha miundo mbinu ya shule za msingi katika shule 61 ifikapo Juni 2019 | Fedha zilizotolewa ni kidogo sana | 15 |
| | Kuongeza kiwango cha ufaulu wa watoto wa darasa la Nne na Saba kutoka asilimia 70 hadi 95 ifikapo Juni 2019 | Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi waliofanya mtihani wa taifa wa darasa la 4 ni asilimia 91 na kwa darasa la saba ni asilimia 67 | 82 |
| | Kuhakikisha uandikishaji wa watoto kujiunga na darasa la kwanza kinaongezeka kutoka asilimia 89 hadi asilimia 98 ifikapo Juni 2019 | Uandikishaji wa watoto wa darasa la kwanza umefikia asilimia 77 | 77 |
| MAENDELEO YA JAMII | Kuhakikisha shughuli za kujitegemea za kuongeza kipato | Hakuna fedha | 0 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | cha mwananchi zinaanzishwa | | |
| | Kutoa fedha asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa miradi ya vijana na akina mama ifikapo Juni 2020 | Jumla ya vikundi 13 vya vijana na akina mama vimepatiwa mkopo kati ya vikundi 10 vya vijana na vikundi 10 vya akina mama | 50 |
| | Kutoa elimu na huduma kwa wananchi juu ya kujikinga na maambukizi ya HIV/AIDS katika vijiji vyote 72 na kuhakikisha wale walioathirika wanapata matibabu na ushauri nasaha | Kazi ya kutoa elimu na ushauri nasaha kwa watu wanaoishi na virusi pamoja na kujikinga na maambukizi mapya imefanyika kwa njia ya mikutano na sinema kwenye Kata chache | 10 |
| MIFUGO NA UVUVI | Kuimarisha na kuboresha mifugo ili kuongeza thamani ya ngozi na nyama kwa wafugaji wadogo kutoka asilimia 9 hadi 13 na kupandisha uzalishaji zao la nyama kutoka | Kundi moja la akina mama la ujasiriamali wamepata mafunzo juu ya utunzaji wa ngozi za wanyama kwaajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwemo mikoba, mikanda, seti za masofa n.k. mafunzo yalitolewa na UNESCO | 40 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | Tshs 172 Milioni hadi Tshs 330 Milioni ifikapo Juni 2017 | | |
| KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA | Kuongeza thamani ya mazao na kuongeza uzalishaji kutoka asilimia 30 hadi 53 ifikapo Juni 2017 | Hakuna fedha zilizotolewa | 0 |
| USHIRIKA NA MASOKO | Kutoa elimu ya biashara na ushirika kwa vyama vya ushirika vipatavyo 40 ifikapo Juni 2017 | Hakuna fedha zilizotolewa | 0 |
| AFYA | Kuongeza idadi ya kaya zinazojiunga na CHF kutoka kaya 139 hadi 10,000 ifikapo Juni 2017 | Jumla ya kaya 1,198 zimejiunga na CHF | 75 |
| | Kupunguza maambukizi ya HIV/AIDS kutoka asilimia 1.7 hadi 1 ifikapo 2019 | Kiwango cha maambukizi mapya ya HIV kimeongezeka kutoka asilimia 1.3 hadi 1.7 | 0 |
| | Kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 138 | Kazi iliyofanyika ni kupunguza maambukizi ya kifua kikuu na ukoma | 45 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | hadi 100 kati ya 100,000 ifikapo Juni 2019 | | |
| | Kupunguza tatizo la upatikanaji wa madawa na vifaa tiba kutoka asilimia 45 had 35 ifikapo Juni 2019 | Fedha zilizotolewa ni kidogo kazi hazijafanyika | 0 |
| | Kuondoa tatizo la miundo mbinu ya afya katika zahanati na vituo (ujenzi wa zahanati na vituo vya afya) katika kata 28 kutoka asilimia 40 hadi 20 ifikapo Juni 2019 | Fedha zilizotolewa ni kidogo sana , kazi imefanyika kwa asilimia 10 | 10 |
| ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa chini ya program ya SEDP katika shule za sekondari 6 | Fedha zimetolewa kidogo sana na kazi imefanyika kwa asilimia 33 | 33 |
| | Kuongeza kiwango cha wanafunzi cha kufaulu mitihani ya taifa ya kidato cha nne kutoka asilimia 43 hadi 85 ifikapo | Kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa kidato cha 4 na 6 kimepanda kwa asilimia 50 | 50 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | Juni 2019 | | |
| | Kuongeza kiwango cha mahudhurio ya wanafunzi wa sekondari kutoka asilimia 67 hadi 100 ifikapo Juni 2019 | Kiwango cha mahudhurio ya wanafunzi kimeongezeka kutoka asilimia 67 hadi 70 | 5 |
| MAJI VIJIJINI | Kuongeza kiwango cha wananchi wanaopata maji safi na salama katika vijiji 72 kutoka asilimia 58 hadi75 ifikapo Juni 2019 | Asilimia 56 ya wananchi wanaoishi vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama hadi sasa | 56 |
| BARABARA | Kukarabati jumla ya km 140 za barabara za Wilaya ifikapo Juni 2017 | Jumla ya km 88.7 ziko katika hatua ya taratibu za manunuzi | 15 |
| ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA | Kupima mipaka ya vijiji na kutatua migogoro ya ardhi kwa vijiji 10 ifikapo Juni 2017 | Hakuna fedha zilizotolewa | 0 |
| RAMANI NA UPIMAJI | Mpango kabambe wa kufanya savei na kupima maeneo ya makazi katika Kata 28 ifikapo Juni 2019 | Mradi bado haujaanza hakuna fedha | 0 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| WANYAMA PORI | Kuhifadhi maeneo ya wanyamapori katika Kata 28 ifikapo Juni 2020 | Maeneo 360 ya hifadhi ya wanyama pori yametembelewa na kuhifadhiwa | 50 |
| HIFADHI YA MISITU | Kuhakikisha maeneo ya hifadhi ya misitu na mazingira yanalindwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria | Vikao vya kulinda maliasili, misitu na hifadhi vimefanyika katika vijiji 10 vinavyoizunguka misitu iliyohifadhiwa | 50 |
| SHERIA | Kuhakikisha sheria za Mamlaka ya serikali za Mitaa zinaimarishwa katika vijiji 72 ifikapo Juni 2019 | Utawala bora na utii wa sheria unazingatiwa katika Halmashauri | 45 |
| MKAGUZI WA NDANI | Kuhakikisha kwamba matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo yanakagulia na kutolewa taarifa katika vikao vya kisheria, na kamati ya ukaguzi ya wilaya inafanya kazi yake ipasavyo | Ukaguzi umefanyika kwa robo mbili za mwaka wa fedha na ripoti imewasilishwa kwenye menejimenti kwa utekelezaji | 50 |

| HALMASHAURI NA SEKTA | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| TEHAMA NA UHUSIANO WA JAMII | Kuhakikisha kwamba jamii inapata taarifa na mrejesho wa shughuli za Halmashauri kwa kuandaliwa taarifa mbalimbali, pia kuimarisha mahusiano ya kimtandao kati ya Ofisi ya Halmashauri na Katibu Tawala. Pamoja wadu wengine wa maendeleo | Halmashauri imetengeneza mfumo mzuri wa mawasiliano na Taasisi zote zinazohusika | 50 |
| UFUGAJI WA NYUKI | Kuibui miradi ya ufugaji nyuki kwa vikundi vya wananchi katika vijiji vyote 72 ili kuongeza kipato cha wananchi katika kaya ifikapo Juni 2020 | Vikundi vipatavyo 25 vimeanzishwa na jumla ya vikundi 130 vimepatiwa mizinga ya kufugia nyuki ikiwa ni msaada kutoka Frankfurt Zoological Society | 70 |

**Changamoto katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa kipindi cha Julai – Desemba 2016**

1. Kuongezeka kwa bei kiholela kwa baadhi ya vifaa na huduma muhimu kama vile vifaa vya ujenzi n.k.
2. Uitikiaji mgumu wa wananchi katika kuchangia miradi ya maendeleo katika maeneo yao.
3. Uhaba wa mafundi na makontrackta wa ujenzi katika vijiji na kata, ambapo imepelekea miradi mingi kukosa wajenzi wenyeji wa maeneo hayo na kufanya Halmashauri kuingia mikataba na makontrackta wenye uzoefu na ujuzi nje ya wilaya.
4. Ubovu wa barabara unaosababisha ubovu wa mawasiliano hasa nyakati za mvua
5. Tatizo la umeme ambalo halikithi mahitaji halisi ya wilaya.
6. Gharama kubwa za wakandarasi.
7. Uhaba wa watumishi wenye taaluma mbalimbali na wengi waliopo kutopendelea kufanya kazi kwenye mazingira magumu.
8. Ucheleweshaji wa kutolewa kwa fedha kutoka serikali kuu kwaajili ya kutekeleza miradi.
9. Ukame wa mara kwa mara kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ambao unaathiri mazao ya chakula na mifugo.
10. Uhaba wa chakula katika tarafa ya Ngorongoro kutokana na wananchi kutoruhusiwa kufanya shughuli za kilimo katika maeneo ya hifadhi ya mamlaka ya Ngorongoro

**Mikakati ya kutatua changamoto hizo kwa siku zijazo**

1. Kuweka mikakati ya kufuatilia fedha kutoka serikali kuu ili miradi ya maendeleo itekelezwe kwa wakati.
2. Kushawishi na kuhamasisha wananchi ili wawe na moyo wa kujitolea.
3. Kuhakikisha miradi midogomidogo inaunganishwa na kupewa kipaumbele ili kumpata mkandarasi mmoja mwenye sifa atakayefanya kazi kubwa.
4. Kufanya ukarabati wa mara kwa mara wa barabara za vijijini.

5. Mpaka sasa Shirika la Umeme Tanzania limeweka umeme katika eneo la Loliondo na Wasso, hivyo jitihada zinaendelea kuhakikisha maeneo mengine ya Mji wa Loliondo yanapata umeme wa REA mapema.

6. Kuhakikisha maandalizi ya document za tenda zote yanaandaliwa mapema ili fedha znapoletwa hasa ikiwa zimechelewa, inakuwa rahisi kwa Halmashauri kutangaza tenda zake na kutumia fedha kwa wakati unaofaa.

7. Kujenga nyumba za watumishi katika maeneo ya Kata na Vijiji ili kupunguza tatizo la nyumba za watumishi na kuwawezesha watumishi kuwa na mazingira mazuri ya kuishi hata kama wapo katika maeneo yenye mazingira magumu.

8. Kuhakikisha miundo mbinu ya mifugo ikiwemo majosho, mabwawa na vibanio yanaboreshwa, ili kutengeneza maeneo ya upatikanaji wa malisho bora na kupunguza uharibifu wa mazingira, hii ni pamoja na kuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi katika vijiji na kata zote za Ngorongoro.

9. Kuwapatia chakula kaya zote zilizoathirika na ukame hasa zile kaya ambazo zinapakana na hifadhi, ambako wananchi wamekatazwa kufanya shughuli za kilimo kwaajili ya kuhifadhi mazingira ya wanyama pori

**HALMASHAURI YA MERU**

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| MAJI ( miradi ya LGCDG) | Kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama unaongezeka kutoka watu 1,500 kwa sasa hadi 5,000 ifikapo Juni 2017 | Ujenzi wa skimu 4 za maji katika vijiji vya Njoro, Poli, Nkoarisambu na Akheri haujafanyika, fedha hazijatolewa | **0** |
| | Kuboresha mazingira ya | Kukamilisha ujenzi wa jengo la Halmashauri ili | **0** |

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | kufanyia kazi kwa watumishi ifikapo Juni 2017 | watumishi waweze kupata ofisi za kutosha, kazi haijafanyika kwasababu fedha haijatolewa | |
| Programu ya LGCDG | Kuboresha huduma za kilimo, mifugo, biashara na utalii | Ujenzi wa soko la Tengeru, Machinjio Tengeru na kituo cha utalii usariver, kazi hizi hazijafanyika kwa sababu ya fedha hazijatolewa | **0** |
| | Kuhakikisha miundombinu ya masoko inaboreshwa ifikapo Juni 2017 | Ujenzi wa miundombinu katika stand ya basi mbuguni haujatekelezwa kutokana na fedha kutotolewa | **0** |
| | Kukarabati na kukamilisha ujenzi wa barabara ifikapo Juni 2017 | Ujenzi wa barabara za Leguruki – Ngarananyuki<br>Kikatiti – Makiba,<br>Leganga – Songoro<br>Kazi hizi hazijafanyika kutokana na fedha kutotolewa | **0** |
| | Kufanya ukarabati mdogo wa | Ukarabati mdogo wa barabara hizo bado | **0** |

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | barabara ya Malti – kwasadala Majengo – Relini<br><br>Ubungo – Ndoombo<br><br>Ifikapo Juni 2017 | haujafanyika, kutotkana na kutotolewa fedha zake | |
| | Kukamilisha ujenzi wa daraja la Olkungw"adu | Daraja la Olkung"wadu limejengwa na kukamilika | **100** |
| | Kufanya ukarabati wa barabara ya Aloyce km 7 ifikapo Juni 2017 | Kazi ya ukarabati wa barabara haijafanyika kutokana na fedha kutotolewa | **0** |
| | Kufanya ukarabati wa barabara ya Seela – Sing'isi Km 10 ifikapo Juni 2017 | Kazi ya ukarabati haijafanyika kutokana na fedha kutotolewa | **0** |
| ELIMU MSINGI<br><br>FEDHA ZA LGCDG | Kuhakikisha miundombinu ya shule za msingi inaboreshwa kwa kujenga vyumba vya madarasa, vyoo na nyumba za walimu ifikapo Juni 2017 | Ujenzi wa vyoo 15 katika shule za msingi haujafanyika, hakuna fedha zilizotolewa | **0** |
| | | Ujenzi wa wa vyumba vya madarasa 30 na | **0** |

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | nyumba za walimu 12 haujafanyika kutokana na fedha kutototolewa | |
| ELIMU YA SEKONDARI | Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga vyumba vya madarasa 30, Bwalo la chakula, nyumba za walimu na maabara | Ujenzi wa vyumba 30 vya madarasa katika shule za sekondari haujafanyika kutokana na kukosekana kwa fedha | **0** |
| | | Ujenzi wa Bwalo la shule ya sekondari Shishiton haujaanza kutokana na kutototolewa kwa fedha | **0** |
| | | Ujenzi wa nyumba za walimu 12 haujafanyika kwa sababu fedha hazijatolewa | **0** |
| | | Ujenzi wa maabara 19 katika shule za sekondari umekamilika katika shule 6 na shule 13 bado ujenzi wa maabara unaendelea | **58** |
| Programu ya NRSSP | Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa | Ujenzi wa mradi wa bomba kwa ajili ya | **0** |

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | maji safi na salama na kuhifadhi maji taka kutoka watu 185,610 hadi 193,019 ifikapo Juni 2017 | maji salama na huduma ya uhifadhi wa maji taka katika kijiji cha Mikungani haujafanyika kwa sababu fedha hazikutolewa | |
| MIPANGO | Kuhakikisha uratibu na ufuatiliaji wa miradi na shughuli zingine za maendeleo zinatekelezwa ifikapo Juni 2017 | Kazi ya ukaguzi wa miradi na uandaaji wa ripoti imefanyika kwa wakati na ripoti imewasilishwa | **50** |
| | Kuwepo kwa mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa watumishi kwa kujenga ofisi za kata na vijiji na kuweka samani | Ujenzi wa ofisi za Kata ya Makiba na Kingori haujaanza kutokana na kukosekana kwa fedha | **0** |
| | Kutoa mafunzo kwa mahakama za kata juu ya wajibu wao na kutenda kazi zao kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria katika kutoa haki kwa wananchi | Mafunzo ya siku mbili imetolewa kwa mahakama za kata kutokana na mapato ya ndani | **25** |

**Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo**

1. Kucheleweshwa kwa fedha za miradi na matumizi ya kawaida kutoka serikali kuu ambapo kwa mwaka 2015/2016 Halmashauri imepokea asilimia 36.10 kati ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
2. Fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya sekta ya Kilimo ni ndogo sana pamoja na kwamba Kilimo ndio uti wa mgongo, bado serikali haijaweza kuangalia kwa undani zaidi suala la kilimo pamoja na kile cha umwagiliaji.
3. Baadhi ya miradi kutopewa fedha kabisa pamoja na kwamba sekta hizo zimeandaa bajeti zao kwa mwaka wa fedha husika (mfano Mifugo, uvuvi na umwagiliaji).
4. Uhaba wa watumishi katika fani ya Mipango, Elimu, Maendeleo ya Jamii, Kilimo na Maafisa vijiji na Kata

**Mipango Mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo kwa siku zijazo**

1. Halmashauri ya Meru imeandaa mpango wa mda mfupi katika kuhakikisha inakusanya mapato yake ya ndani kwa ufanisi.
2. Katika mipango yake ya mda mrefu Halmashauri imejipanga kuendelea na ujenzi wa eneo la biashara katika mji wa Useriver (Business centre) karibu na makao makuu ya wilaya, pia ujenzi wa Kituo cha kisasa cha mabasi na malori yanayokwenda masafa marefu katika eneo la Madiira katika Barabara Kuu ya Arusha – Moshi, kwa ajili ya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato

**HALMASHAURI YA ARUSHA**

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| MAJI | Kuhakikisha idadi ya wananchi wanaopata maji safi na salama | Asilimia 62 ya wananchi wa Halmashauri ya Arusha wanapata maji | 62 |

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | wanaongezeka kutoka asilimia 56 hadi 70 ifikapo Juni 2017 | safi na salama | |
| ELIMU MSINGI | Kuhakikisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanaboreshwa ifikapo Juni 2019 | Ujenzi wa nyumba 15 za walimu bado haujaanza kutokana na fedha kutotolewa | 0 |
| | Kuhakikisha mazingira ya kujifunzia yanaboreshwa kwa kujenga vyumba 40 katika vijiji 21 ifikapo Juni 2019 | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 9 kati ya 40 vimejengwa na kukamilika, na ujenzi wa vyumba vya madarasa 23 vipo katika hatua mbalimbali ya ujenzi | 30 |
| ELIMU YA SEKONDARI | Kuhakikisha mazingira ya kujifunzia yanaboreshwa ikiwemo kukarabati maabara, vyoo na nyumba za walimu katika shule za sekondari 22 ifikapo Juni 2019 | Ukarabati wa nyumba za walimu umeanyika kwa kukarabari nyumba 1 yenye unit sita (ina uwezo wa kuchukua walimu 6), vyoo 20 vyenye matundu 10 vimekarabatiwa na kukamilika | 60 |
| | Kuhakikisha ukaguzi wa shule unafanyika | Jumla ya shule 52 za sekondari zilikaguliwa | **100** |

| SEKTA/PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | katika kila robo ya mwaka ya utekelezaji | katika maeneo ya ufundishaji, taaluma na nidhamu | |
| MAENDELEO YA JAMII | Kutoa huduma kwa makundi ya watu wanaoishi na virusi vya ukimwi, wajane na wagane katika Kata 21 ifikapo Juni 2017 | Makundi 5 ya watu wanaoishi na virusi vya ukimwi wamepewa huduma ikiwemo fedha kwa ajili ya kuboresha afya zao | 60 |
| | Kuwatembelea majumbani watu 100 wanaoishi na virusi vya ukimwi ifikapo Juni 2019 | Watu 20 wanaoishi na virusi vya ukimwi wametembelewa na kupatiwa huduma na ushauri nasaha | 80 |
| MIFUGO | Kuendeleza na kukarabati miundo mbinu ya mifugo 5 katika Kata 3 | Kazi hazijafanyika kutokana na kukosa fedha | 0 |
| MIPANGO NA URATIBU | Kuhakikisha miradi ya maendeleo inakaguliwa na kufanyiwa tathmini ifikapo Juni 2017 | Ukaguzi na tathmini ya miradi umefanyika katika kata 27 | 100 |

**Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia Julai 2016 hadi Desemba 2016**

1. Gharama kubwa za ufuatiliaji katika kukusanya kodi na tozo mbalimbali za Halmashauri.

2. Kuchelewa kupata fedha na wakati mwingine kupewa fedha kidogo kutoka serikalini kwa ajili ya matumizi mengineyo na zile za miradi ya maendeleo ambako kumesababisha miradi mingi kushindwa kutekelezwa kwa wakati.

3. Magonjwa kama vile HIV/AIDS , sukari na shinikizo la damu yanayowakabili baadhi ya wananchi katika Kata na Vijiji yamechangia sana kupunguza nguvu kazi inayotegemewa katika sekta mbalimbali za uzalishaji.

4. Mapato madogo yanayokusanywa kutokana na baadhi ya vyanzo kukosa Wazabuni wakukusanya katika maeneo hayo ambayo Halmashauri imeyaona ni gharama sana kukusanya wenyewe kwa kutumia watumishi wa Halmashauri

**Mikakati ya baadae ya kukabiliana na changamoto hizo na utatuzi wake**

1. Ili kuweza kufikia malaengo ya Halmashauri, mikakati iliyowekwa ni pamoja na kufanya tathmini upya kwa vyanzo vyote vya mapato, ili kubaini ni vyanzo vipi vitaipatia faida Halmashauri kwa kuendelea kuwepo na kukusanywa. Hii itasaidia sana kupunguza mlolongo wa vyanzo ambavyo ni gharama kwa Halmashauri katika ukusanyaji wake kwani havilipi hata nusu ya gharama za ukusanyaji.

2. Baadhi ya vyanzo vya mapato vitabinafsishwa na kuongezwa viwango, ili atakayepewa tenda hiyo akusanye kulingana na viwango vitakavyowekwa na Halmashauri baada ya kufanya tathmini upya. Mfano ushuru wa masoko na stendi za mabasi.

3. Kuhakikisha elimu zaidi inaendelea kutolewa katika maeneo yote ambayo HIV/AIDS bado kiwango chake ni kikubwa kulingana na takwimu zilizopo, aidha watumishi wa Halmashauri wataendelea kushirikiana na wananchi katika sekta zao kila wanapotembelea Kata na Vijiji kutoa ujumbe juu ya athari za UKIMWI na maambukizi yake.

4. Halmashauri itaendelea kutumis watumishi wake katika kukusanya mapato ya ndani kwa yale maeneo yatakayokosa mzabuni

**HALMASHAURI YA LONGIDO**

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| UTAWALA | Kuhakikisha kunakuwepo na mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa watumishi pamoja na kuwalipa stahiki zao za kisheria ifikapo Juni 2017 | Stahiki za kisheria za watumishi 189 zimelipwa ikiwemo kulipa na posho za likizo, tuition fees, malipo ya posho za masaa ya ziada, safari za kikazi na gharama za mazishi | 36 |
| | Kuhakikisha shughuli zote za Halmashauri zinatekelezwa kwa mujibu wa Kanuni na sheria ikiwemo kuendesha vikao vya kisheria na kulipa stahiki za viongozi ifikapo Juni 2017 | - Posho za mwezi kwa waheshimiwa Madiwani zimelipwa<br><br>- Taarifa za kila robo za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri na maendeleo ya miradi kwa miezi 6 zimeandaliwa na kuwasilishwa katika vikao, na vikao vya menejimenti vimefanyika pia katika miezi 6 | 79 |
| SHERIA | Kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma | Kati ya kesi 5 ambazo zinaikabili Halmashauri, kesi 3 | 79 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | nzuri za kisheria kuanzia kwenye Vijiji, Kata mpaka Halmashauri ifikapo Juni 2017 | zimemalizika kutatuliwa bado 2<br>Halmashauri ina mkakati wa kuwa na Mahakama zenye uwezo ndani ya Kata pindi fedha zitakapopatikana | |
| MKAGUZI WA NDANI | Kuhakikisha Halmashauri inakuwa na Hati safi ya ukaguzi ifikapo Juni 2017 | Mfumo wa kukusanya mapato umeshawekwa na unatumika na Halmashauri imo katika maandalizi ya kukamilisha sera ya udhibiti wa ndani wa mapato | 78 |
| FEDHA NA BIASHARA | Kuhakikisha kwamba mapato ya Halmashauri yanapanda kutoka Tshs 1,289,505,700 mwaka 2015 hadi Tshs 1,359,504,700 ifikapo Juni 2017 | Hadi kufikia Desemba 2016 mapato ya Halmashauri yalifikia Tshs 400,105,344 sawa na asilimia 30. Halmashauri inafanya jitihada kubwa ikiwemo kutathmini upya vyanzo vipya vya mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato | 30 |
| MIPANGO, | Kuhakikisha | 1. Ushirikishwaji wa | |

| **SEKTA/ PROGRAMU** | **SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA** | **UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016** | **ASILIMIA YA UTEKELEZAJI** |
|---|---|---|---|
| TAKWIMU NA UFUATILIAJI | ushirikishwaji wa wananchi kuanzia ngazi ya chini katika kupanga mipango ya maendeleo na ufuatiliaji katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ifikapo Juni 2017 | wananchi wakati wa kuandaa bajeti 2017/2018 umefanyika katika Vitongoji 175, Vijiji 40 na Kata 18<br><br>2. Usimamizi wa matumizi ya fedha za (2015/2016) zilizovuka mwaka ziliendelea kutumika 2016/2017 pamoja na miradi mingine na shughuli zote zingine zilitekelezwa katika vijiji 29.<br><br>3. Taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa wakati kwenye Wizara husika<br><br>4. District Social Economic Profile ya | **50** |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | mwaka 2016/2017 ilifanyiwa marekebisho | |
| KILIMO, MIFUGO NA UVUVI | Kuimarisha huduma za ugani katika Kata 18 ifikapo Juni 2017 | 1. Wafugaji wapatao 2169 katika Kata 18 walitembelewa na kupewa ushauri<br><br>2. Chanjo ya mifugo imetolewa kwa mifugo 324,124 kazi hii imefanyika kwa ushirikiano na mradi wa Maisha Bora | **40** |
| | Kuhakikisha ngome wanaboreshwa na kuongeza thamani ya zao hili | Uzito wa ngombe wa kilo 250 kwa sasa unatarajiwa kuongezeka hadi kilo 500 ifikapo Juni 2017 baada ya Halmashauri kununua madume bora 10 na kuyagawanya katika vikundi 3 vya wafugaji kwa kuanzia. Aidha Halmashauri inaendelea | **30** |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kuboresha mifugo ya kiasili | |
| KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA | Kuhakikisha kwamba kiwango cha uzalishaji wa mazao kilichopo sasa kinaongezeka kwa ekari kufikia tani 1.2 kwa ekari ya maharage na tani 1.8 ya ekari ya mahindi ifikapo Juni 2017 | 1. Maandalizi ya awali yanaendelea katika kuboresha na kuanzisha FFS kwa ajili ya zao la maharage ya Soya na Alizeti katika vijiji 4. Fedha kwa ajili ya kazi hii hazijatolewa mpaka sasa | 5 |
| ARDHI | Kuhakikisha kwamba umiliki wa ardhi kwa mwananchi unaongezeka kutoka watu 500 hadi 1,500 ifikapo Juni 2017 | Umilikishaji wa ardhi umefanyika kwa watu 100 wenye viwanja, ingawaje fedha hazijatolewa na serikali | 40 |
| UFUGAJI NYUKI | Kuhamasisha wananchi kuendelea kufuga nyuki kisasa ili kupata mazao yatokanayo na nyuki kwa wingi katika Kata 3 ifikapo Juni 2017 | Elimu imetolewa kwa wafugaji<br><br>Wa nyuki kutumia mizinga ya kisasa katka kata 1. Fehda pia haijatolewa kwa ajili ya kazi hii | 40 |
| MAJI | Kuhakikisha kwamba kila mwananchi anpata maji safi na | 1. Ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 9 | 50 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | salama na kwamba kiwango cha huduma hiyo kinapanda kutoka asilimia 48 ya sasa hadi asilimia 68 ifikapo Juni 2017 | inaendelea<br><br>2. Ujenzi wa mabwawa 2 ya maji katika Kata ya Kiserian na Engikareti yanaendelea kukamilishwa. Aidha ucheleweshaji wa fedha umesabaisha miradi hii kutokamilika kwa wakati | |
| AFYA | Kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vifaa vya uchunguzi vinaongezeka kutoka asilimia 60 ya sasa hadi 80 ifikapo Juni 2017 | Usambazaji wa madawa, vifaa tiba umefanyika kwa vituo vya afya 3, na zahanati 26. Pia lipo duka dogo la MSD limeanzishwa katika kituo 1 cha afya ili kurahisisha upatikanaji wa dawa | 78 |
| | Kupunguza vifo vya mama kutoka vifo 116 kati ya wajawazito 100,000 hadi vifo 100 kwa wajawazito 100,000 ifikapo Juni 2017 | 1. Kliniki za mkoba zinaendelea kuhudumia vijiji 24 ambavyo havina huduma ya afya<br><br>2. Huduma ya Uzazi wa Mpango imeendelea kuwafikia | 50 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | wananchi katika vijiji 10 | |
| | Kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 32 kati ya watoto 1000 wanaozaliwa hadi vifo 20 kati ya watoto 1000 wanaozaliwa ifikapo Juni 2017 | 1. Usambazaji wa chanjo na IUD kwa zahanati 24 umefanyika<br>2. Usambazaji wa chanjo kwa vituo vya afya 3 umefanyika<br>Halmashauri inaendelea na jitihada zake za kuhakikisha chanjo pamoja na matone ya vitamin A yanatolewa kwa watoto wote chini ya umri wa miaka 5. Kazi ya uhamasishaji inaendelea | 50 |
| | Kuhakikisha tatizo la malaria linapungua kutoka asilimia 14 ya wagonjwa wa malaria hadi asilimia 10 ifikapo Juni 2017 | 1. TN kwa ajili ya vituo vya afya 3 na zahanati 24 imetolewa kwa idadi ya paketi 120<br>2. Kipimo cha MRDT kwa ajili ya kupima malaria imetolewa | 40 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | kwa vituo vya afya 24<br><br>3. Uhamasishaji kwa wananchi juu ya matumizi ya vyandarua umefanyika katika vijiji 49<br><br>Aidha Halmashauri imeendelea kuhamasisha wananchi juu ya kujiunga na CHF | |
| HIV/AIDS | Kuhakikisha maambukizi ya HIV/AIDS yanapungua kutoka asilimia 2.9 ya sasa hadi asilimia 2.2 ifikapo Juni 2017 | Hadi kufikia Desemba 2016 kiwango cha maambukizi kimepungua kutoka asilimia 2.9 hadi asilimia 2.1 ilipofika Desemba 2016 | |
| | Kuhakikisha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa afya na mabwana afya pamoja na menejimenti ya Hospitali yanaboreshwa kutoka asilimia 40 ya | Ukaguzi shirikishi umefanyika katika vituo vya afya 24, ikiwemo kukagua ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo hivyo, uwepo w madawa, na uwepo wa watumishi wa kada zote | 50 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | sasa hadi 70 ifikapo Juni 2017 | wanaofanyakazi kwa kuzingatia maadili. | |
| | Kuhakikisha miundo mbinu ya huduma za afya inaongezeka kwa kuwa na ongezeko la zahanati kutoka 25 hadi 30 na vituo vya afya 2 hadi 6 ifikapo Juni 2017 | Ukarabati wa zahanati 1 umefanyika na ujenzi wa chumba cha X-ray unaendelea katika kituo cha afya, ingawaje fedha za kukamilisha bado kutolewa | 52 |
| ELIMU YA MSINGI | Kuhakikisha kunakuwepo na mazingira mazuri ya kufanyia kazi ifikapo Juni 2017 | Malipo ya kisheria kwa watumishi ikiwemo nauli na posho ya likizo, gharama za matibabu zimelipwa hadi kufikia 30 Desemba | 43 |
| | Kuhakikisha upatikanaji wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia kwa shule za msingi 41 ifikapo Juni 2017 | Kazi hii ni endelevu, kwani hadi sasa kitabu 1 kinatumiwa na watoto 3. Pia uandikishaji wa watoto kujiunga na darasa la I umefikia asilimia 58 | 33 |
| | Kuhakikisha miundombinu ya shule za msingi inaboreshwa ifikapo Juni 2017 | Mpaka sasa ujenzi wa vyumba vya madarasa 12 na nyumba 4 unaendelea, hata | 26 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | hivyo zaidi ya nyumba 302 na vyumba vya madarasa 188 vinahitajika | |
| | Kuhakikisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa msingi kinapanda kutoka asilimia 38 hadi 61 ya mwaka 2015, asilimia 70 ya mwaka 2016 na asilimia 78 ifikapo mwaka 2017 | 1. Kiango cha ufaulu wa darasa la saba kimeongezeka kutoka asilimia 50 hadi 69 ya mwaka 2016<br><br>2. Kiwango cha ufaulu kwa darasa la Nne kimeongezeka kutoka asilimia 63 hadi 87 mwaka 2016<br><br>Viwango hivi vimefikiwa kutokana na jitihada za makusudi za kuboresha miundombinu ya | 52 |
| | Kupunguza kiwango cha kutokujua kusoma na kuandika kutoka asilimia 50 ya sasa hadi asilimia 40 ifikapo Juni 2017 | Madarasa ya elimu ya watu wazima 10 ya mpango wa COBET yametembelewa na kukaguliwa | |
| ELIMU YA SEKONDARI | Kuhakikisha kunakuwepo na | gharama zote za kisheria ikiwemo | 56 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia kwa walimu na wanafunzi ifikapo Juni 2017 | mishahara, likizo, usafiri na gharama za ofisi zimelipwa | |
| | Kuongeza kiwango cha ufaulu kwa mtihani wa Kidato cha IV kutoka asilimia 70 hadi 75, Kidato cha IV kutoka asilimia 85 hadi 95 na Kidato cha VI kutoka asilimia 94 hadi 100 | Kiwango cha ufaulu katika mtihani wa Taifa kidato cha II kimeongezeka kutoka asilimia 85 hadi 91<br><br>Kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Taifa kidato cha IV kimefikia asilimia 67 na kwa Kidato cha VI kiwango cha ufaulu kimepanda kutoka asilimia 94 hadi 98 mwaka 2016<br><br>Ufaulu huu umetokana na jitihada zilizofanywa na sekta katika kuwapa motisha walimu ambao shule zao zimefanya vizuri ili kuweza kuwapa hamasa ya kuendelea | |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | kufanya vizuri zaidi | |
| | Kuhakikisha mazingira ya shule za sekondari yanaboreshwa kwa kuweka mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia kwa fedha za Capitation ifikapo Juni 2017 | Kiasi cha Tshs 116,375,000 zimepokelewa na kupelekwa kwenye shule za sekondari 8 kwa ajili ya kununulia vitabu na vifaa vingine vya kufundishia | 30 |
| | Kuendelea kukarabati miundombinu ya shule 6 za sekondari ifikapo Juni 2017 | 1. Ujenzi wa vyumba vya maabara 22 katika shule 8 za sekondari ziko katika hatua ya kukamilika na maabara 3 zimekamilika<br>2. Ujenzi wa nyumba 6 za walimu na vyumba 12 vya madarasa unaendelea<br>Aidha Halmashauri inaendelea na jitihada zake za makusudi kuweza kukamilisha maabara 19, kujenga zaidi ya vyumba vya madarasa 58 kwa | 45 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | kuwashirikisha wananchi na wadau wengine wa maendleo katika bajeti ya mwaka 2017/2018 | |
| MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO | Kufanya ukaguzi shirikishi na kuwahamasisha Vijana na Akina Mama, wazee na mashirika yasiyo ya kiserikali kuanzisha vikuni vya uzalishaji na kupata kipato ifikapo Juni 2017 | 1. Ufuatiliaji wa miradi ya vikundi umefanyika katika vikundi 10 vya vijana na akina mama<br>2. Mafunzo juu ya ujasiriamali yametolewa kwa vikundi 10 vya akina mama na vijana. | 50 |

**Changamoto zilizojitokeza wakati wa kutekeleza shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia Julai 2016 hadi Desemba 2016**

1. Changamoto kubwa ni kucheleweshwa kwa fedha za miradi ya maendeleo ambapo ilipofika Juni 2016 Halmashauri ilikuwa imepokea Tshs 1,162,215,128 sawa na asilimia 14 kati ya Tshs 7,820,323,156 kwaajili ya miradi ya maji iliyokuwa ikiendelea katika vijiji 10. Aidha fedha zilizoidhinishwa hazikidhi mahitaji muhimu ya Halmashauri hivyo kufanya shughuli nyingi kutokamilika kwa wakati. Miradi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, miradi ya maji, ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya na ujenzi wa vyumba vya madarasa ya sekondari yote hii inahitaji fedha nyingi ili kuweza kukamilika

**Mikakati ya kupambana au kutatua changamoto hizo kwa siku zijazo**

1. Kutafuta fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo NGOs na Wizara husika kwaajili ya ujenzi wa mabwawa ya maji, kufanya miradi ya kuvuna maji ya mvua wakati wa masika, kuendeleza ujenzi wa vyanzo vipya vya maji, na kukarabati miundombinu ya maji iliyopo ili iweze kutoa huduma hiyo.
2. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kufanya tathmini upya ya vyanzo hivyo na kuvibinafsisha ili kuepuka mianya ya wizi wa mapato na udanganyifu
3. Kuendelea kufanya upembuzi yakinifu (feasibility study) juu ya vyanzo vya maji .
4. Kutengeneza mazingira mazuri na shughuli kwa ajili ya kuvutia watalii na wawekezaji na kuanzisha WMA na kuboresha barabara na miundombinu mingine ikiwemo upatikanaji wa maji katika maeneo yenye vivutio.
5. Kuwezesha watumishi zaidi juu ya matumizi ya EPICOR pamoja na IPSAS ili kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha kwa kuzingatia mfumo wa udhibiti matumizi ya serikali kulingana na bajeti.
6. Kutumia rasilimali zilizopo katika kujiletea maendeleo kwa kushirikiana na sekta sisizo rasmi na sekta binafsi na wadau wengine katika kutekeleza miradi ya maendeleo endelevu.
7. Kuwa na matumizi mazuri ya nishati mbadala kama vile sola katika mashule, zahanati na nyumba za watumishi, ili kupunguza matumizi makubwa ya umeme

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| KILIMO | Kuhakikisha eneo lote linalofaa kwa kilimo linatumika kwa kuongeza eneo kutoka hekta 3,234 hadi hekta 6,000 ifikapo | Kazi haikufanyika kutokana na kukosa fedha | 0 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | Juni 2019 | | |
| | Kuongeza kiwango cha mazao ya ngombe kwa kuboresha mifugo hiyo kwa muda wa miaka 3 katika vijiji 62 | Kazi hazijaanza kutokana na kukosa fedha | 0 |
| | Kuhakikisha mifugo yote inapata chanjo zote muhimu dhidi ya magonjwa makuu ya mifugo na mlipuko kwa vijiji 62 ifikapo 2019 | Kazi haijafanyika kutokana na kukosa fedha | 0 |
| | Kuongeza uzalishaji wa mazao makubwa yanayolimwa katika maeneo husika kwa tani kwa ekari katika vijiji 62 ifikapo Juni 2019 | Kazi hazijaanza kutokana na kukosa fedha | 0 |
| | Kujenga uwezo kwa maafisa ugani 64 katika wilaya ili kuwapa uwezo wa kuhudumia wakulima 19,000 kwa ufanisi zaidi ifikapo Juni 2019 | Kazi hii haijaanza kutokana na kukosekana kwa fedha | 0 |
| | Kuviendeleza na kuviunganisha vikundi vya SACCOS katika Kata 20 ili kuendesha miradi midogo midogo yenye kuinua kipato | Kazi hazijaanza kutokana na kukosa fedha | 0 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | Kuboresha zao la ngozi linalotokana na mifugo ya wafugaji ili kulipandisha hadhi kutoka asilimia 25 ya sasa hadi asilimia 80 ifikapo Juni 2019 | Wafugaji 60 na wadau wengine wamepewa mafunzo juu ya kuhifadhi vizuri ngozi za mifugo<br><br>Watengenezaji wa ngozi 40 wanaotumia ngozi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali wamepata mafunzo juu ya kutunza ngozi za asili za wanyama<br><br>Ukarabati mdogo umefanyika katika machinjio ya Mto wa Mbu na Monduli Mjini ili kuyafanya yawe na ubora unaotakiwa. | 58 |
| MAENDELEO YA JAMII | Kuhakikisha vikundi vya uzalishaji mali vya akina mama 35 na vijana vinapewa mbinu na uwezo wa kujiendeleza na kujipatia fedha | Vikundi 5 vya wanawake na watu wazima kutoka katika kata 2 vimepata mafunzo ya ujasiriamali, wakati | 32 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | vikundi 5 vya wanawake katika kata 3 vimepata mafunzo | |
| | Kutoa ufadhili kwa watu wanaoishi na virusi, wajane na wagane katika kata 20 ifikapo Juni 2019 | Fedha hazijatolea hivyo kazi haijafanyika | 0 |
| MAJI | Kuhakikisha jamii inapata maji safi na salama kwa kupandisha kiwango kutoka asilimia 63 ya sasa hadi asilimia 85 ifikapo Juni 2019 | Mpaka sasa Halmashauri imeshampata mtaalam mshauri na ameshafanya kazi zifuatazo<br>1. Ushauri wa kitaalam umeshatolewa kwa vijiji 10 vilivyochaguliwa,<br>2. Ujenzi umeanza katika kijiji cha Lolkisale<br>3. Kazi za kuchimba kisima kirefu na vifupi imeanza katika eneo la Magereza katika kijiji cha Moita | ,Kazi zote zimefikia asiklimia 86 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | 4. Andiko la mwisho kwa ajili ya mradi wa maji imeshaandaliwa kwa ajili ya bwawa moja<br><br>5. Masuala ya afya na utunzaji wa maji yamefundishwa katika vijiji 2 na shule 2 za msingi<br><br>6. Vyoo vya mfano 30 vimejengwa katika vijiji 10 vilivyochaguliwa ndani ya mradi<br><br>7. Kazi za usimamizi, ufuatiliaji na tathmini zimefanyika katika mradi huu ikiwa ni pamoja na kufanya matengenezo ya | |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | vyombo vya usafiri vya idara husika kwa ajili ya ufuatiliaji | |
| ELIMU YA MSINGI | Kuhakikisha kiwango cha ufaulu wa darasa la saba kinaongezeka kutoka asilimia 60 hadi 95 ifikapo Juni 2019 | Kiwango cha ufaulu kimepanda na kufikia 63.6 kwa wanafunzi waliofanya mtihani wa kitaifa wa darasa la 4 na 7 | 63 |
| | Kuhakikisha kwamba watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa ifikapo Juni 2017 na kwamba kiwango cha uandikishaji kinapanda kutoka asilimia 65 hadi 95 | Wanafunzi walioandikishwa wamefikia asilimia 94 | 94 |
| | Kuhakikisha kiwango cha kutojua kusoma na kuandika kinapungua kutoka asilimia 33 hadi 18 ifikapo Juni 2019 | Kiwango kimefikiwa kwa asilimia 125 cha kupunguza wasiojua kusoma na kuandika sawa na watu 220 katika mpango wa COBET na watu 725 katika mpango wa CBAE | 125 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| ELIMU SEKONDARI | Kiwango cha Kuandikisha watoto wa kidato cha kwanza kipande kutoka ailimia 82 hadi 95 ifikapo Juni 2019 | Wanafunzi wote waliofaulu mtihani wa Taifa wa darasa la saba wamechaguliwa na kujiunga na kidato cha kwanza | 100 |
| | Kuhakikisha kiwango cha ufaulu katika mitihani ya taifa ya kidato cha !!, IV na VI vinaongezeka kutoka asilimia 48 hadi 75 | Kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa kidato cha IV kimepanda na kufikia asilimia 62 | 62 |
| BARABARA | Kuhakikisha barabara zenye urefu wa km 149 zinapitika wakati wote ifikapo Juni 2019 | 1. Ukarabati wa barabara ya mji wa Monduli unafanyika mara kwa mara<br>2. KM 5 za barabara ya Monduli – zimefanyiwa matengenezo madogo<br>Barabara ya Monduli – Arkaria – Mti mmoja km 23 zimefanyiwa | 65 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | matengenezo madogo- | |
| AFYA | Kuongeza huduma za afya kwa kuhakikisha zinawafikia wananchi wengi kutoka asilimia 44 hadi 80 ifikapo Juni 2019 | 1. Wakunga wa jadi katika wilaya ya Monduli walitambuliwa na kuhamasishwa juu ya uzazi salama wa wateja wao na kuwafikisha katika vituo vya afya pindi wanapojifungua kwa uchunguzi zaidi<br><br>2. Wananchi katika kata 20 pia walielimishwa juu ya umuhimu wa kujifungulia katika zahanati au kituo cha afya. | 72 |
| | Kuhakikisha matone ya vitamin A na dawa za minyoo yanatolewa kwa watoto chini ya miaka 5 kwa asilimia 93 hadi 94 | Matone ya Vitamin A pamoja na dawa za minyoo vimetolewa kwa watoto chini ya miaka 5 kwa | 95 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | asilimia 95 | |
| | Kila mgonjwa anapata huduma ya ART ifikapo Juni 2019 | Maeneo ya kutolea huduma ya CTC yameongezeka kutoka 6 hadi 7<br><br>Maeneo ya huduma ya PTTC yameongezeka kutoka 5 hadi 6<br><br>Maeneo ya kupima kwa kutumia huduma mashine ya CD4 yameongezeka kutoka 1 hadi 3 | 49 |
| | Kuhakikisha kwamba angalao asilimia 60 ya zahanati na vituo vya afya vinahudumia wagonjwa wenye magonjwa ya zinaa ifikapo Juni 2019 | Vituo vya huduma ya afya 25 (87) vinatoa huduma ya kutibu magonjwa ya zinaa pamoja na elimu ya kujikinga<br><br>Dawa za kupima magonjwa haya zimesambazwa | |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | katika vituo vya huduma | |
| | Kuhakikisha chanjo ya DPT-HepB-Hib na ile ya surua inatolewa kwa zaidi ya asilimia 90 ifikapo Juni 2019 | Jumla ya route 20 (46%) kati ya 44 zimepangwa kwa ajili ya kutembelea vijijini kwa kutumia klinik za mkoba<br><br>Maeneo 21(48%) kati ya 44 yanayoweza kufikiwa na huduma za afya yamefikiwa<br><br>Chanjo ya PENTA 3 imeongezeka kutoka asilimia 89 hadi 91 | 75 |
| | Kuhakikisha kwamba angalao asilimia 30 ya wananchi wanafikiwa na kupea elimu juu ya NCDs ifikapo Juni 2019 | Kata 7 kati ya 15 wananchi wake wamepatiwa elimu na matibabu ya magonjwa ya macho | 47 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| FEDHA | Kuhakikisha kwamba malipo yote ya kisheria yanafanyika kwa wakati | 1. Malipo ya ukarabati na gharama za kiutendaji yamefanyika kwa asilimia 87<br><br>. | 87 |
| | Kufanya mafunzo ya kitaalamu kwa watumishi ifikapo Juni 2019 | Watumishi 2 wamepatiwa mafunzo ya komputa<br><br>Watumishi 2 wapo kwenye mafunzo ya masuala ya fedha | 51 |
| | Kuhakikisha taarifa za utekelezaji na matumizi ya fedha kila robo mwaka zinataarishwa na kuwasilishwa ifikapo Juni 2017 | Taarifa 6 za utekelezaji na matumizi ya fedha ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa wahusika | 50 |
| | Kuhakikisha manunuzi ya Halmashauri yanafanyika kwa kufuata utaratibu na kanuni zake | Manunuzi yamefanyika kwa sekta mbalimbali ikiwemo huduma mbalimbali kwa Halmashauri kutoka kwa | |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | wazabuni<br><br>Halmashauri pia ina mpango wa mwaka wa manunuzi | |
| UTAWALA | Kuhakikisha kiwango cha utoaji huduma muhimu kwa watumishi kinaongezeka kutoka watumishi 211 to 324 ifikapo Juni 2019 | 1. Jumla ya watumishi 34 wenye sifa wameajiriwa katika sekta za elimu na afya<br><br>2. Watumishi 212 wamepewa motisha katika utendaji wao wa kazi ikiwemo kupandishwa vyeo na kulipwa stahiki zingine za kisheria<br><br>3. Ujenzi wa ofisi za Kata 2 zimejengwa<br><br>4. Ofisi 10 za Kata | 78 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | zimepewa vifaa ikiwemo viti na meza awamu ya pili kwa lengo la kujenga mazingira bora ya kufanyia kazi<br><br>5. Vikao vya kisheria vya kata vimefanyika na kuratibiwa<br><br>6. Stahiki za watumishi zimelipwa kwa wakati | |
| | Kuhakikisha vikao vya kisheria vya Menejimenti vinaongezeka na kufikia 60 kwa mwaka | Vikao vya kila mwezi na vile vya robo ya mwaka vimefanyika katika miezi hii 6 | 50 |
| | Kuhakikisha elimu inatolea kwa watumishi na wananchi juu ya kupambana na rushwa ifikapo Juni 2019 | Kamati za kupambana na rushwa katika sehemu za kazi na kwenye vijiji na kata katika wilaya zimeimarishwa | 45 |
| SHERIA | Kuhakikisha huduma za | - Kuhudhuria kesi zote zinazohusu | 50 |

| SEKTA/ PROGRAMU | SHUGHULI NA LENGO KWA MWAKA | UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUANZIA JULAI 2016 HADI DESEMBA 2016 | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | kisheria zinatolewa kwa wananchi na watumishi ifikapo Juni 2019 | Halmashauri na kuzitetea<br>- Kutoa mafunzo kwa Mahakama za Kata<br>- Kulipa stahiki za kisheria kwa Mwanansheria wa Halmashauri | |
| UTAWALA BORA | Kuhakikisha mafunzo ya ndani yanatolewa kwa watumishi na Waheshimiwa Madiwani juu ya Kanuni, Taratibu na Sheria za kuendesha Halmashauri ifikapo Juni 2019 | Waheshimiwa Madiwani wamepatiwa mafunzo juu ya Utawala Bora unaozingatia sheria | |
| | Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi kwa kununua vitendea kazi | Komputa 1 na vifaa vyake imenunuliwa pamoja na stetonary | 70 |

**Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia Julai 2016 hadi Desemba 2016**

1. Kucheleweshwa kwa fedha za miradi ikiwemo fedha za usimamizi na ufuatiliaji ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangia miradi kutokaguliwa kwa wakati.
2. Uhaba wa vitendea kazi ikiwemo Komputa mpakato (laptops).
3. Kukatika kwa umeme mara kwa mara ambako kunasababisha taarifa na kazi za kiofisi kutokamilika kwa wakati.

4. Kutokuwepo kwa Takwimu sahihi katika baadhi ya sekta za Halmashauri ambapo imekuwa vigumu kwa idara ya Mipango na Uratibu kuwa na takwimu sahihi wakati inapoandaa taarifa mbalimbali zinazohitaji takwimu.

5. Hakuna fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya DADPS kwa kipindi cha miaka 3 ingawaje serikali imekuwa ikituagiza kuweka miradi hiyo katika bajeti kila mwaka.

6. Uhaba wa wataalamu katika Taasisi za binafsi katika kufanya savei ya maeneo ya umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa, umesababisha miradi mingi kuchelewa kutekelezwa kwa wakati.

7. Upungufu wa wakandarasi wenye sifa katika maeneo ya Vijijini.

8. Uwezo mdogo wa wananchi katika kuchangia fedha na nguvu zao kwenye miradi ya maendeleo iliyopo katika maeneo yao.

9. Ukame wa mda mrefu ulioukumba Wilaya

    - Uhaba wa fedha za kuwalipa wakandarasi
    - Uwezo mdogo wa Halmashauri katika kuchangia miradi ya maendeleo ambao umesababisha miradi mingi kuchelewa kutekelezwa kwa wakati

10. Kuchelewa kuidhinishwa kwa fedha za miradi ya Barabara, ambayo inategemea makubaliano kati ya PO-RALG na Halmashauri imesababisha miradi mingi kuchelewa kutekelezwa na mingine kufikia wakati wa kipindi cha mvua na utekelezaji kuwa mgumu.

11. Uchache wa fedha za barabara zinazotolewa na serikali, kwa sasa yupo mfadhili mmoja anayetoa fedha katika program hii ya barabara (Road Funds).

12. Uhaba wa miundombinu katika shule za sekondari ikiwemo vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na vyoo

**Mikakati iliyowekwa kutatua changamoto hizi kwa siku zijazo**

1. Kuhakikisha Halmashauri inafuatilia mara kwa mara upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na serikali.

2. Kutenga bjeti kwa ajili ya kununua vifaa vya ofisi ambavyo ni lazima kwa umuhimu wake.

3. Kununua genereta kubwa ambalo litatumika wakati umeme unapokatika ili kuweza kukidhi mahitaji ya Halmashauri, haswa kipindi kunapokuwepo na mgao wa umeme..

4. Kuhakikisha kila sekta inakuwa na mfumo mzuri wa kutathmini takwimu zake na kuzitunza, na vilevile Halmashauri imetengeneza mfumo wa jumla wa kutunza takwimu (Data base) ambao utapunguza shida ya kutokuwa na takwimu sahihi.

5. Serikali iwe inatoa fedha iliyoahidi hasa katika miradi ambayo inagusa maisha ya wananchi ili huduma hizo ziweze kupatikana kwa wakati.

6. Kuhakikisha Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji inajengewa uwezo ili iweze kutoa elimu kwa ofisi za Halmashauri za umwagiliaji juu ya masuala ya umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa madogo, hii ni pamoja na kuajiri wahandisi wa umwagiliaji na wahandisi wasaidizi katika ngazi ya Halmashauri na pia wakati mwingine kuomba msaada wa wahandisi kutoka Halmashauri zingine.
7. Kuunganisha tenda ndogondogo zinazofanana ili kuweza kumpata mkandarasi mmoja atakayetekeleza kazi hizo kuliko kuwa na wakandarasi wengi kwa kazi zinazofanana.
8. Kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wao katika kuchangia maendeleo ndani ya maeneo yao.

9. Halmashauri zitafute vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya barabara kuliko kungoja fedha za wafadhili ambao wakati mwingine hutoa fedha kwa masharti magumu ambayo Halmashauri zinashindwa kutekeleza. Mfano mzuri ni kutenga fedha katika mfuko wa CDG, TASAF na n.k fedha ambazo tayari serikali imekuwa na uhakika wa kuzipata.

10. Serikali iendelee na kutoa fedha kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya shule za sekondari ya kujenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na vyoo, kupitia katika mpango wake wa SEDP. Aidha wananchi pia wachangie nguvu zao zaidi katika kazi ambazo wanaweza kuzifanya na kuokoa fedha ambayo ingeweza kutumika katika kuanza ujenzi wa jingo lingine (ikiwemo kuchimba msingi, kuchota mawe, kusafisha eneo la ujenzi na kupanga tofali).

**KIAMBATANISHO NA. 2**

## MAPENDEKEZO YA BAJETI 2017/18 - SEKRETARIETI YA MKOA WA ARUSHA KWA KILA SEKSHENI NA VITENGO

| FUNGU | KIASI | DEVELOPMENT | FOREIGN |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 12,162,318,000 | | |
| 1001 – UTAWALA | 644,225,200 | 624,364,000 | |
| 1002 – UHASIBU | 40,464,000 | 0 | |
| 1003 – UKAGUZI WA NDANI | 18,000,000 | 0 | |
| 1004 – MANUNUZI | 12,000,000 | 0 | |
| 1005 – DAS ARUSHA | 40,000,000 | 0 | |
| 1006 – DAS NGORONGORO | 40,000,000 | 0 | |
| 1007 – DAS KARATU | 40,000,000 | 0 | |
| 1008 – DAS ARUMERU | 40,000,000 | 0 | |
| 1009 – DAS MONDULI | 40,000,000 | 0 | |
| 1010 – DAS LONGIDO | 39,759,540 | 680,000,000 | |
| 1014 – SHERIA | 9,119,000 | 0 | |
| 1015 – TEHAMA | 12,324,000 | 0 | |
| 2001 – MIPANGO | 96,339,200 | 40,000,000 | 65,800,000 - HIV |
| | | | 45,000,000 - CDG |
| 2002 – UCHUMI | 39,008,280 | 0 | |
| 2003 – MIUNDOMBINU | 45,910,000 | 0 | |
| 2005 – SERIKALI ZA MITAA | 36,663,200 | 0 | |
| 2006 – ELIMU | 279,103,000 | 0 | |
| 2007 – MAJI | 24,800,000 | 81,515,731 | |
| 3001 – HOSPITALI | 492,600,000 | 1,736,537,000 | |
| **JUMLA** | **14,152,633,420** | **3,162,416,731** | **110,800,000** |
| **JUMLA KUU** | | **17,425,850,151** | |